ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.

46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tatu – Tarehe 22 Januari, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: (Kny: Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nidhati na Ardhi, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Sera ya Nishati ya Zanzibar.

Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Sera ya Nishati ya Zanzibar.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 106

Utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza:-

Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu imepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuridhiwa na Baraza la Wawakilishi.

(a) Sheria hiyo inasema kuwa Makao Makuu ya Shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu yatakuwa Zanzibar. Je, ni hatua zipi zilizochukuliwa kutekekeleza matakwa hayo ya kisheria.

(b) Zanzibar imegawiwa kiasi gani cha samaki waliokamatwa kwenye meli ya kigeni ambayo ilikuwa ikivua kwenye bahari ya Tanzania kinyume cha sheria na Mahkama kuamuru samaki hao wagawiwe kwa taasisi mbali mbali za huduma Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake, naomba nitowe ufafanuzi ufuatao:-

Mhe. Spika, Sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu imepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini bado mpaka sasa hivi haijaletwa Barazani kwa ajili ya kuridhiwa.

Mhe. Spika, baada ya ufafanuzi huo, naomba kutoa jibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) hatua zilizochukuliwa kutekeleza matakwa haya ya kisheria ni kama hizi zifuatazo:-

- Ofisi ya Muda ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu tayari imeshafunguliwa hapa Kinazini Zanzibar katika jengo la ZSTC.

- Utaratibu wa kujengwa Ofisi za Kudumu unaendelea na michoro ya Ujenzi huo ipo tayari, kwa sasa hivi hatua ya kumpata mjenzi ipo katika hatua za mwisho. Ofisi hio inatarajiwa kujengwa huko Fumba katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

(b) Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepewa mgao wa samaki kwa mujibu wa mgao wa mapato kama Sheria za Uvuvi wa Bahari Kuu zilivyoainisha (yaani asimilia 40). Kutokana na hali halisi tuliyonayo hivi sasa ya kukosekana kwa Umeme, Serikali tumeshindwa kupokea samaki hao kwa vile itakuwa ni vigumu kuwahifadhi na kuweza kuwasafirisha kidogo kidogo kuwaleta hapa Zanzibar. Ili kuondoa gharama zaidi za uhifadhi wa samaki hawa, serikali imeona ni vyema samaki hao kugaiwa kwa taasisi zitakazojitokeza kwa mujibu wa mahitajio yao huko Tanzania Bara.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, Mhe. Waziri amelieleza Baraza hili kuwa sheria hii bado haijaridhiwa na Baraza la Wawakilishi. Matakwa ya Katiba yanazungumza sheria hiyo ambayo kama inataka kutumika kwa sehemu zote mbili ifanywe hivyo.

(a) Je, ni lini italetwa hapa na hivi sasa watu wameshaanzisha afisi hiyo hapa Zanzibar.

(b) Samaki Mhe. Spika, tutasema Mhe. Waziri ametunyima, kwa sababu kiasi hicho cha samaki wangekuja tu leo wakapiga hesabu basi kila mwananchi angepata samaki wake hapa bila kuharibika. Samaki aliyekaa kwenye barafu ya aina ile basi anaweza kukaa mpaka siku tatu. Kwa hivyo, samaki wetu tungeletewa sote hapa kwa muda huo niliozungumza Mhe. Spika, tungeweza kugaiwa kwenye vituo vyetu vya wagonjwa na wananchi tukapata. Haoni kama hivyo Mhe. Waziri wametudhulumu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, swali lake (a) ameuliza kwamba sheria hii ya Uvuvi wa Bahari Kuu bado haijaridhiwa hapa Barazani kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, ameuliza ni lini italetwa ili kuweza kuridhiwa.

(a) Mhe. Spika, nataka nimthibitishie Mhe. Haji Mkema Haji kwamba taratibu zinaendelea na sheria ile wakati wowote itapelekwa kwenye Baraza la Mapinduzi kwa kupata baraka na baadae itakuja hapa kwa ajili ya kuridhiwa.

Mhe. Spika, kwa sababu katika marekebisho ya sheria ile, kwa kuwa na sisi tuliwahi kupata kutoa maoni mbali mbali.Kwa hivyo, tunategemea yale yaliyokubaliwa ndio haya ambayo kwa mfano mgao wa 60 kwa 40 na mambo mengine ya makao makuu kujengwa wapi.

Kwa hivyo, mambo mengi kwa kweli yamefanywa katika hali ya mashirikiano. Kwa hivyo, kitu cha msingi kilichobakia ni kukamilisha tu zile taratibu za kisheria. Hilo tunategemea asaa kheri kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na pengine labda Mhe. Waziri muhusika anaweza kutoa ufafanuzi, nadhani katika kikao kinachokuja inaweza ikaja, lakini hilo nitamuachia Mhe. Waziri baadae nikishakaa azidi kunisaidia kutoa ufafanuzi.

(b) Mhe. Spika, Mhe. Haji Mkema Haji amesema kwamba samaki hao kutokuwaleta hapa tunawadhulumu wananchi. Mhe. Spika, hatuwadhulumu wananchi, tunawapenda sana wananchi wetu na ndio maana serikali kila kitu inachokifanya inabidi itumie busara za hali ya juu. Samaki wale sio samaki fresh, ni samaki ambao wamevuliwa muda mrefu wameshakaa huko baharini zaidi ya miezi sita, tokea walipovuliwa huko baharini wakapelekwa Mahakamani, wameshakaa zaidi ya miezi sita mingine. Kwa hivyo, ni zaidi ya mwaka mmoja samaki wale wanahangaishwa, mara wanaingizwa huku na kutolewa huku.

Vile vile, Mhe. Spika, samaki wale sio kama unakwenda kutaka kila 20 unatiliwa tu, kuna jokofu maalum la kuweza kuwasafirisha samaki wale. Vile vile, kuna gharama kubwa sana za kuweza kuwasafirisha, kwa sababu hicho chombo kuweza kukikodi yaani *coldroom container*, inabidi uwasafirishe kwa wingi na ukishafika hapa lazima uwe na hifadhi maalum. Vinginevyo Mhe. Spika, tunaweza tukenda kuvamia samaki, matokeo yake tukajakumpa kazi Mhe. Mugheiry kwa ajili ya matumbo ya kuharisha. Kwa hivyo, ndio maana serikali ikajaribu kuangalia kwa makini sana ili kuweza kulinda afya za wananchi wetu.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali mawili ya nyongeza.

(a) Samaki hawa sisi kitu ambacho tunapata ni asilimia 40.Kwa hivyo, ni samaki wengi sana. Lakini kwa kutilia maanani kwamba samaki hawa wakati wote huo walikuwa wamewekwa katika barafu. Kwa hivyo, bado watakuwa wana barafu. Je, hatuoni kwamba samaki hawa wangeletwa wangekuwa bado barafu yao imo kama wale mbuzi wanaoletwa kutoka Makka na wameshatumia zaidi ya mwaka mmoja.

(b) Mhe. Spika, ikiwa kama kweli serikali ilikuwa na azma ya kuwasaidia Wazanzibari. Kwa nini samaki hawa wasiwauze kule kwa taasisi zinazohusika ili fedha zile tukazipata sisi Wazanzibari hapa kwa kuwapa hizo taasisi kama hospitali na mwahala mwingine mnamohusika. Kwa hivyo, swali ni kwamba kwa nini wasiuze ili tukapata fedha badala ya wao kugawa samaki kwa watu ambao wao wameshapewa samaki wao. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe amesema kwamba kwa kuwa samaki wale wako kwenye barafu mpaka wakifika hapa bado wataendelea kuwa na barafu, na akatoa mfano kama mbuzi wa Makka.

(a) Mhe. Spika, mbuzi na kondoo wa Makka wanapoletwa hapa, wanaletwa kwenye kontena lake mpaka pale bandarini. Kwa hivyo, ina maana mpaka wameshafika kwenye bandari ya Zanzibar bado wako katika kile chombo walichohifadhiwa. Kama nilivyosema kwamba samaki hawa ambao wako kule Tanzania Bara, sasa hivi wako kwenye *coldroom*, lakini pale wanapotolewa inabidi lazima kipatikane chombo chengine cha kuweza kuwahifadhi na kuwaleta huku. Kwa hivyo, hapo kuna gharama kubwa sana.

Nafikiri Mhe. Spika, kama Waheshimiwa Wajumbe watakuwa wanafuatilia sasa hivi wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameshatumia zaidi ya milioni mia moja kwa ajili ya ule utaratibu wa kuwatoa samaki hapa na kuwapeleka hapa ili kuwahifadha na mambo mengine mbali mbali. Kwa hivyo, na sisi tunaweza tukaingia gharama kubwa ya kuanza kuwachukua samaki wale na matokeo yake wakajakuharibika, huku serikali imeshakula gharama na wananchi wakajakupata athari vile vile. Ndio maana tuko makini sana.

Mhe. Spika, mpaka sasa hivi kama tulivyosema bado hatujawachukua, lakini tunataka kushauriana na wenzetu kwamba wale samaki ikiwezekana basi zigaiwe zile taasisi kule kule Tanzania Bara ili kuepusha hasara ambayo inaweza ikajitokeza ya fedha, lakini na afya za watu.

(b) Mhe. Spika, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ametoa wazo la kuweza kuwauza samaki wale kule Tanzania Bara ili zile fedha zije kusaidia jamii. Mhe. Spika, Waziri muhusika wa uvuvi alizungumza kwamba samaki wale watatolewa bure kwa taasisi zile ambazo za jamii. Kwa mfano kama Magereza, Vikosi na katika mashule mbali mbali.

Mhe. Spika, sisi tukienda kuuza ina maana kwanza tutakuwa tunamkiuka mwenzetu kwa ule ushauri ambao ameutoa. Kwa hivyo, hili bado tutajaribu kuchukua huu ushauri, lakini tutashauriana na wenzetu, kama watatukubalia tuwauze sawa. Lakini kule wenzetu wamepewa bure, sasa sisi tukiuza sijui. Suala hili tunalichukua na tutajaribu kulifanyia kazi, kama kutakuwa kuna uwezekano huo tutafanya. Bado hatutegemei kwamba samaki wale kwa agizo lililotoka kuwa wagaiwe, sisi tukiuza tunaweza tukajakuonekana tumekwenda kinyume na taratibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweka ufafanuzi mdogo, lakini kabla ya hapo namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, suala hili la Mhe. Abubakar Khamis Bakary, hasa hili linalosema kwamba samaki wale wauzwe halafu pesa zile zingetufaa hapa. Mhe. Spika, napenda kukuhakikishia kwamba suala hili tulikuwa tukilifuatilia kwa kina sana na maamuzi yaliyotoka sio ya Waziri wa kule, ni maamuzi ya Mahakama kwamba hao samaki watolewe bure kwa taasisi husika. Kwa hivyo, wenzetu kule wameshaanza na wanatoa bure. Kwa hivyo, nafikiri sisi itakuwa hatuwezi kuwauza, hata kama tutawachukuwa lakini hatuwezi kuwauza, kwa sababu maamuzi yameshatoka na Mahakama kwamba samaki wasiuzwe watolewe bure. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kuona umuhimu mkubwa wa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe Spika, kesi hii nzima inayohusiana na samaki hawa Mhe. Spika, imetawaliwa na imegubikwa na utata mkubwa. Hasa pale inapotolewa tafsiri ya Zanzibar na its territorial. Kwa maana hiyo kutokana na hilo wale samaki kwa asilimia mia moja walikuwa ni wa Zanzibar. Sasa nitoke huko niseme kwamba hiyo sheria ambayo inazungumzwa hapa anayosema Mhe. Waziri kwamba haijaletwa katika Baraza hili kwa kuridhiwa bado inakuwa ni batili na kwa sababu ni batili na zile taratibu zinazoendelea za kujenga afisi na mengineyo, naona zote zilipaswa kutokuendelea mpaka hapo sheria hiyo itakapoletwa hapa.

(a) Sasa je, Mhe. Waziri huoni kuendelea na hayo ambayo umesema yanafanyika hapa mnataka kuihalalisha kinyemela sheria hii na kufanya hivyo ni kuinyima haki Zanzibar kwa sababu itaathiri na vitu vyengine.

(b) Mhe. Spika, kuhusiana na mgao huo ambao mimi nasema ni wa maiti ya samaki, kwa sababu hawakuwekwa bado katika hali ile ile ambayo tunasema wangekaa katika barafu yake ya tangu mwanzo basi wasingefika kuambiwa kwamba wanataka kuharibika, wamewekwa wapi na wapi. Naomba radhi, lakini tafsiri yangu mimi nawaita ni maiti wa samaki.

Je, ni kigezo gani kilichotumika kuambiwa Zanzibar tupewa asilimia 40, lakini mambo mengine yote ya Muungano tukapewa asilimia 4.5, hili limetokea wapi na ilikuwaje hasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, sikubaliani na Mhe. Zakiya Omar Juma kwamba sheria hii ni batili kwa kuwa bado haijaridhiwa na Baraza la Wawakilishi. Kwa sababu Mhe. Spika, kama unavyofahamu kwamba kuna sheria nyingi ambazo zilikuwa zikitungwa na huwa zinafanyakazi mpaka Zanzibar lakini bado zilikuwa hazijaridhiwa na bado zilikuwa zinaendelea kutumika.

(a) Mhe. Spika, kwa busara zetu na hasa kupitia katika hivi vikao vya Mhe. Waziri Kiongozi na Mhe. Waziri Mkuu vinavyosimamiwa na Makamu wa Rais, kwamba imekuwa ikisisitizwa sana kuwa tujaribu kuangalia upya sheria zetu zile ambazo zinazohitaji kufanyiwa marekebisho, ili zifanye kazi bila ya utata basi ziweze kufanyakazi kwa vizuri na yale mambo madogo madogo tuweze kuyarekebisha.

Mhe. Spika, ndio maana sasa hivi hili suala la uvuvi wa bahari kuu baada ya marekebisho yote yale yaliyofanyika, kwamba sasa hivi tayari utaratibu umeshaanza kwamba itakuja nategemea kwamba wakati wowote italetwa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kupata hiyo ridhaa. Kwa hivyo, bado sheria hii kwa kuwa tayari imeshapitishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sio batili na hizi taratibu zote ambazo zinazoendelea sasa hivi bado sio kuwa ni batili. Lakini kama vile tulivyozungumza, tunajitahidi kukamilisha zile taratibu ili haya mambo sasa yaende bila ya kuwa na utata wa aina yoyote.

(b) Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma, amesema kwamba hii ni maiti ya samaki. Nafikiri samaki wote tunaowala wanakuwa sio wazima wote wanakuwa wameshakuwa marehemu ndio tunawala. Kwa hivyo, nafikiri hili pia lisiwatie wasi wasi kwa sababu kuna wengine wanaweza wakashtuka wakiambiwa marehemu samaki wakamtupa. Kwa hivyo, hao marehemu samaki wote wanapaswa kuliwa na hutakiwi umle mzima, maana yake ukimla mzima sasa ndio utakuwa unamdhulumu. Kwa hivyo, mimi nafikiri Mhe. Zakiya Omar Juma asiwe na wasi wasi kwamba hawa samaki bado ni halali kuliwa.

Vile vile, ameeleza kwamba kwa mujibu wa sheria yetu hii mgao wote wa Muungano tunapata asilimia 4.5. Kwa nini suala la huu mgano wa samaki kupitia hii sheria ya uvuvi wa bahari kuu ikawa tumepata asilimia 40.

Mimi nafikiri Mhe. Zakiya Omar Juma kwanza alikuwa ampongeze Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira hapa Zanzibar. Kwa sababu ni jitihada kubwa ambayo iliyofanywa na wenzetu wa Idara ya Uvuvi, kuweza kutetea hoja hii ya msingi na wakashiriki katika vikao mbali mbali na wakajenga hoja. Hoja yao ilivyoonekana kuwa ni ya msingi na ukiangalia Zanzibar ni visiwa na mazingira ya visiwa, nafikiri ni moja katika vigezo vilivyotufanya kwamba katika suala hili zima la uvuvi wa bahari kuu basi tuweze kupata asilimia 40 na wenzetu wapate asilimia 60.

Mhe. Spika, kwa kweli ilikuwa sio kazi ndogo, ilikuwa ni kazi kubwa na ninasema kwamba nataka tuwapongeze wenzetu hawa, kwa sababu kwanza waliifanya kwa nia njema kabisa na wenzetu walipokaa nao kule wakaridhiana. Nafikiri na taasisi nyengine ukiacha Idara ya Uvuvi na wengine kama wakikaa kuangalia hasa kinadharia hali halisi ilivyo wakafanya maamuzi kama haya, basi nadhani wangetuletea faraja kubwa sana.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Zakiya Omar Juma asiwe na wasi wasi kwamba huu mgao wa asilimia 40 ni vikao ambavyo walivyokaa baina ya Idara ya

Uvuvi Zanzibar pamoja na wenzetu Tanzania Bara. Walipoona zile hoja za Zanzibar ni za msingi, basi wakakubaliana hii hoja ya kwamba Zanzibar tuweze kupata mgao wa asilimia 40 na wenzetu wapate asilimia 60. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 74

Maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Duniani

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Katika kila mwaka ifikapo tarehe 10/12/2009 ulimwengu huadhimisha siku ya Haki za Binadamu Duniani. Hapa Zanzibar siku hii husherehekewa kwa lengo la kutoa taaluma kwa jamii. Kwa mwaka huu siku hiyo ilibeba ujumbe usemao "Binadamu wote huzaliwa Huru. Kemea mambo yote ya ubaguzi"

(a) Mhe. Waziri, kwa kuwa Wizara yako ndio inayoratibu sherehe hizo, tangu kuanza kwake wizara imefanya utafiti wowote kujua kama imesaidia kuleta mwamko kwa jamii kuhusu umuhimu wa haki za binadamu kuenziwa.

(b) Tume ya Haki za Binadamu inafanya kazi zake vipi hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kutoa majibu kwanza naomba kuanza kwa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba ifikapo kila tarehe kumi ya kila Mwaka Ulimwengu huadhimisha siku ya Haki za Binaadam Duniani. Jamhuri ya Muungano ya Tanzania imeanza utaratibu wa kuadhimisha siku hiyo kuanzia mwaka 2008 ambapo msimamizi wa shughuli nzima ni Tume ya Haki za Binaadamu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mwaka wa 2009 shughuli hiyo ilifanyika hapa Zanzibar na wizara yangu kupitia Idara ya Uratibu Utawala Bora ikawa ni msimamizi mwenza katika shughuli hiyo ambayo kama alivyozungumza Mhe. Mwakilishi ilibeba ujumbe wa 'Binaadamu Wote Huzaliwa Huru, Kemea Mambo Yote ya Ubaguzi'.

(a) Mhe. Spika, wizara yangu haijafanya utafiti wa kitaalamu kuhusu kupima mwamko wa jamii, kuhusu umuhimu wa Haki za Banaadamu

kuenziwa. Hata hivyo, ipo sura na dalili zinazoonesha kwamba shughuli hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kuifanya jamii iendelee kubadilika na kuwa na mwamko. Hali hii inatokana na elimu, shamrashamra, matangazo na hotuba mbali mbali za viongozi kwa jamii katika maandalizi na hatimaye siku ya kilele.

(b) Mhe. Spika, Tume ya Haki za Binaadamu inafanyakazi zake hapa Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu 131. Aidha, Sheria Nam. 7 ya mwaka 2001 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora, kifungu cha 6 cha sheria hiyo kimeweka wazi kazi za Tume. Pia, ufanyaji kazi huo wa Tume hapa Zanzibar unafanyika kupitia Sheria Nam. 12 ya 2003 iliyopitishwa na Baraza lako tukufu. Sheria hii imeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kwa Tume kufanya kazi hapa Zanzibar, kwani imeweza kuipa uwezo wa kisheria kufanya kazi hapa Zanzibar, au kwa maneno mafupi imeridhiwa.

Sheria Nam. 12 ya 2003 ya Zanzibar iliotoa nguvu za kisheria kwa Tume kufanya shughuli zake hapa Zanzibar, kifungu Nam. 1 cha sheria hiyo kimemtaka Waziri anaeshughulikia masuala ya Haki za Binaadamu kuitangaza tarehe husika ya kuanza matumizi ya sheria hiyo ya kuipa uwezo Tume. Hili limefanyika kupitia *Legal Notice* Nam. 31 na kuitaja tarehe 30th April, 2007 kuwa siku ilioanza rasmi Tume kufanya kazi Zanzibar.

Mhe. Spika, Sheria Nam. 8 ya mwaka 2006 ya marekebisho ya Sheria mbali mbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndio iliyomtaja Waziri wa Zanzibar anaeshughulikia masuala ya Haki za Binaadamu kuwa na jukumu la kuwasilisha ripoti ya Tume katika Baraza lako Tukufu.

Aidha, Mawaziri wanaohusika katika masuala ya Haki za Binaadamu ni yule wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, wana jukumu la kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, siku hii ya tarehe 10 mwezi wa 12 wa kila mwaka ikifika huwa ni siku ambayo imeelezwa lengo lake kuwa ni siku za Haki za Binadamu na kujua matatizo na maendeleo mbali

mbali katika nchi kuwa watu wanaishi vipi. Hasa tukitegemea kwamba binadamu wote ni sawa, hajaliwi mtu kwa rangi, kabila wala dini.

Mhe. Spika, swali langu liko hapa. Je, kwa kuwa Mhe. Waziri Idara hii ya Haki za Binadamu ipo hapa kwetu katika nchi yetu hii ya Zanzibar, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuridhiwa na Baraza letu hili la Wawakilishi. Kwa kuwa anasema tathmini bado hawajafanya. Je, wananchi atawaeleza nini juu ya kuhakikisha kwamba sherehe hizi zinasherehekewa kila mwaka lakini tathmini bado haijafanywa, anatoa wito gani kwa wananchi ili waifahamu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, sherehe imeanza mwaka jana mwaka 2009 ndio kwanza imeanza, imeandaa ratiba na imefanya mambo mengi tu kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi kujua umuhimu wa siku hii. Kufanya tathmini ni suala ambalo baada ya kufundisha sasa ndio unafanya tathmini ya uelewa. Kwa hivyo, nadhani kitu muhimu tuendelee na hii sherehe na tutizame namna wananchi watakavyokuwa wanaifahamu vizuri Haki za Binadamu na kupata uelewa, basi hapo ndio itakuwa tathmini inaweza kufanyika wakati huo.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, nakushukuru na namshukuru sana Mhe. Waziri, *counter party* wangu kwa majibu mazuri. Hata hivyo, napenda nimuulize maswali ya nyongeza kama ifuatavyo; Mhe. Spika, kwa kuwa katika semina tuliyofanyiwa Mbweni na wale watu wa APRM katika ripoti yao tuliona mazuri tuliofanya katika Utawala Bora na mapungufu yetu vile vile walitubainishia katika ile *executive summary* ukiangalia utaona wameorodhesha kwa ufupi yale mazuri yetu na mabaya yetu.

(a) Je, tokea ripoti ile kutolewa Mhe. Waziri amejipanga vipi kujisafisha kwa yale mapungufu ambayo yameonekana.

(b) Mhe. Spika, kwa kuwa mijadala mingi inayoendelea hapa Barazani ya pande zote mbili, yameonesha kwamba kuwa bado hali ya Vyuo vya Mafunzo ni mbaya na kuna ukiukwaji wa Haki za Binadamu. Je, yuko tayari afanye ziara anichukuwe na mimi tukatembelee Vyuo vya Mafunzo siku moja, ili tukajionee hali halisi.

(c) Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe amesema kwamba uelewa tayari umeanza kujengeka kwa kiasi fulani. Mimi nakubaliana naye, lakini Mhe. Spika, kuanzia *level* ya juu, yaani juu mpaka kufikia uwakilishi tumeanza kuelewa nashukuru *alhamdulillah* sihaba, lakini tukiangalia viongozi wenzetu walioko chini bado hawajaelewa.

Je, huoni Mhe. Waziri ni vyema kuvishauri hivi vyombo vinavyoshughulikia masuala ya Haki za Binadamu pamoja na wizara yake ikateremka chini kuanzia labda kwenye Wilaya mpaka kwenye Shehia, kwa ajili ya kutoa elimu, kwa sababu juhudi yetu viongozi haina maana ikiwa walioko chini yetu hawafahamu.

Kwa hivyo, atakubaliana na rai yangu hiyo ya kutoa elimu hasa kwa Masheha, Wakuu wa Wilaya pamoja na wafuasi wao.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, madhumuni ya kukubali Tanzania kushiriki kwenye APRM ni kutoa nafasi ya sisi kujipima wenyewe. Kwa kweli hivi juzi imetoka ripoti ya kwanza, ambayo imeonesha pale tulipofanikiwa na penye kuhitaji marekebisho.

Kwa hivyo, bila ya shaka serikali yetu ifanye jitihada ya kurekebisha yale ambayo yanahitaji kurekebishwa. Kwa maana hiyo, inshaallah Mwenyezi Mungu akipenda tutaendelea kulifanyia kazi na kuliona.

Pili, amenieleza kuhusu suala la Magereza. Mhe. Spika, ripoti kuhusu hali ya Magereza ninazo. Kwa hiyo, Magereza *cello* kwenye vituo vya polisi pamoja na mambo mengine na watu wangu wanazo.

Kwa kweli sisi kazi yetu ni kuwashauri wanaohusika, yaani Idara ya Magereza kurekebisha suala lile pamoja na Idara ya Polisi kufikiria masuala ya *cello* wanazowaweka watu. Kwa sababu hivi sasa si wakati tena kuendelea kutumia mtondoo, isipokuwa ni wakati wa kuwajengea watu sehemu maalum pamoja na kwamba wamewekwa pale ndani, lakini wawe katika hali nzuri.

Sasa hiyo, ni kazi ambayo Mhe. Spika, wizara yangu inaifanya. Isipokuwa kama anatamani tukatembee na tukaangalie kile kilichopo, basi mimi nikotayari tupange siku tu, tukatembee pamoja na kuona hali halisi, lakini najua kwamba ripoti zinaeleza Magereza yanahitaji kurekebishwa kwenye sehemu nyingi.

Mhe. Spika, vile vile, ameeleza kwamba chini bado suala la Haki za Binadamu halijaeleweka. Kwa kweli wizara yangu inajitahidi kutoa hizo taaluma. Kwa mfano kama atafuatilia hivi sasa naendelea kutoa taaluma za Haki za Binadamu kwa vyombo mbali mbali na nimeanza kwa vyombo vya ulinzi na usalama, masheha nao tayari na nitaendelea kwa sababu hivi sasa ni *program*, ambayo inaendelea katika wizara yangu juu ya kuelimisha masuala haya *(Makofi)*.

Nam. 49

Meli iliyobeba Waya wa Umeme kutoka Norway

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Hivi karibuni serikali imepokea waya wa kuvushia umeme kutoka Tanga kwenda Pemba kwa ajili ya kuipatia umeme wa uhakika Pemba.

(a) Ni Meli gani iliyobeba waya huo.

(b) Meli hiyo ilichukua muda gani kutoka Norway hadi Tanzania.

(c) Zipo taarifa kuwa meli iliyobeba waya huu ilishindikizwa na manuari za kijeshi na wanamaji wa Norway.

(d) Je, gharama ya usafirishaji waya huo ni kiasi gani na ililipwa na nani.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, meli iliyobeba waya wa baharini katika Mradi wa Umeme Tanga hadi Pemba inajulikana kwa jina la MV. Skagerak inayomilikiwa na Kampuni ya "Nexans" iliyotengeneza waya huo.

(b) Meli hiyo ilianza safari yake kuanzia Norway tarehe 21/10/2009 na kutia nanga katika pwani ya Tanga tarehe 1/12/2009. Hivyo, safari hiyo imechukua muda wa siku 42.

(c) Meli hiyo ilisindikizwa na manuari za ulinzi za kampuni binafsi zilizokodiwa na Kampuni ya "Nexans" kutoka bahari ya Aden hadi Kenya. Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, meli hiyo imelindwa na meli zetu za Kikosi cha K.M.K.M.

(d) Gharama za usafirishaji wa waya zimo katika gharama za jumla za mradi wenyewe ambayo ni fedha za Norway milioni 400. Mradi huu umefadhiliwa kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ya Norway NOK Milioni 300 = Usd 52.91 Milion,

(ii) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania NOK Milioni 34 = Usd 5.996 Milioni na

(iii) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar NOK Milioni 66 = Usd 11.64 Milioni.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Unguja hivi sasa kuna mpango wa kuingiza waya mwengine kupitia Mradi wa *Millennium Challenge*. Kwa hivyo, huu waya unaotoka Norway umekuwa mwepesi sana kufika. Je, kuna masharti yoyote ya Millennium Challenge kutengeneza waya pengine na badala yake wizara ikafikiria kutengeneza waya huu Norway.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mjumbe arudie swali lake sikulifahamu vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali lako.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, kwa kuwa Unguja kutokana na matatizo ya umeme pamoja na uchakavu wa waya uliopo, kuna mpango wa kuingiza waya mwengine kutoka Dar-es-Salaam hadi hapa.

Je, kuna masharti yoyote ya Mradi wa MCC kuagiza waya sehemu nyengine badala ya wao kufikiria kuagiza kule Norway ambako umechukua muda mdogo tu kuleta waya.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, matayarisho ya mradi wa waya huo mwengine, ambao utakuwa na uwezo wa *megawatts* 100 mara mbili ya huu ambao tunao hivi sasa wenye *megawatts* 45. Kwa kweli utaratibu utakaofuatwa ni wa kutoa *tender* na atakayefanikiwa na hiyo *tender*, sasa yeye ndiye atakayefanya kazi hiyo, inawezekana ikawa ni Norway au nchi nyengine.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nshati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru sana pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa majibu yake mazuri. Lakini nimeona kidogo nitoe majibu ya nyongeza zaidi kutokana na hali tuliyonayo.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa Mradi huu wa Ras Kilomoni hadi Fumba kwa Kisiwa cha Unguja, ratiba ya awali ni kumalizika mwaka 2013. Lakini baada ya kuendelea kupata matatizo haya hapa kisiwani Unguja wiki iliyopita tulikuwa na mazungumzo na uongozi wa *MCC*, kwa bahati nzuri kwa msingi

kwa hatua ya mwanzo tumekubalia kwamba tunaweza kupunguza mwaka mzima kwenye ratiba hiyo *(Makofi).*

Tenders zimeshatolewa na kwa bahati nzuri zimejitokeza kampuni nyingi, kwa bahati nzuri zaidi zile kampuni *cream* za duniani kama tano mpaka sita, ambapo tulitegemea itakuwa ni vyema kwetu kujitokeza, kutokana na ustadi pamoja na uwezo wao mkubwa nazo zimejitokeza *(Makofi).*

Mhe. Spika, *tenders* zinafunguliwa terehe 19 ya mwezi ujao. Kwa kweli matumaini yetu makubwa kwamba tukipata mkandarasi au mtengenezaji mzuri miongoni mwa hao tuliowataja, basi tunaweza kupunguza miezi sita hadi minane zaidi kutokana na uwezo wao mkubwa *(Makofi).*

Kwa hivyo, tunayo matumaini makubwa baada ya mazungumzo hayo ya awali, tunategemea tutakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutoa taarifa ya matumaini kwa wananchi baada ya *tenders* hizo kufunguliwa *(Makofi).*

Lakini masharti aliyozungumzia Mhe. Naibu yapo kwa maana hatuwezi kupendekeza apewe mtu fulani, itategemea na namna atakavyoweza kujitosheleza katika maombi ya *tender* yenyewe pamoja na *Tender Committee*, hivyo *MCC* ndio itakayozingatia nani anayefaa kwa mujibu wa viwango pamoja na taratibu zilizowekwa *(Makofi).* Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 91

Unyanyasaji wa Watoto

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara ina mkakati gani kuliondoa tatizo la unyanyasaji watoto wadogo kwa kuwabaka na kuwaingilia kinyume ya maumbile.

(b) Je, wizara yako inasimamiaje kesi za aina hiyo, ili kuhakikisha haki inapatikana kwa watoto na familia za watoto waliodhulumiwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.91 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, wizara yangu inasikitishwa sana na ongezeko kwa vitendo hivi viovu dhidi ya Watoto. Wizara inaendelea kuchukua hatua mbali mbali za kukabiliana na wimbi hili la unyanyasaji na udhalilishaji wa watoto.

Katika kukabiliana na vitendo hivi, wizara inaendelea na mchakato wa kuandaa Sheria ya Mtoto, sheria ambayo itajumuisha masuala yote ya haki, ulinzi na maendeleo ya mtoto. Tuna imani kwamba baada ya kukamilika kwa sheria hii na kuanza kutumika, vitendo hivi viovu dhidi ya watoto vitadhibitiwa kwa kiasi kikubwa.

Vile vile, wizara imeshirikiana na taasisi nyengine zinazoshughulikia masuala ya watoto. Kwa mfano Idara ya Ustawi wa Jamii, Tume ya Haki za Binadamu, Jumuiya ya Walemavu, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake, Wizara ya Katiba na Utawala Bora, Polisi, Magereza pamoja na raia wema, ili Kuunda Kamati ya Kudumu ya kushughulikia masuala haya ya Ulinzi, Ustawi na Maendeleo ya Watoto kwa jumla.

Wizara pia ilifanya uchambuzi wa sheria zinazohusiana na masuala ya kijinsia na kubaini mapungufu, ili kuweza kuyatafutia ufumbuzi. Kutokana na zoezi hilo, wizara imeandaa vitini vya kusomeshea kwa taasisi zinazohusika na masuala ya wanawake na watoto. Wizara ina imani kuwa matumizi ya vitini hivi yatapunguza vitendo vya unyanyasaji dhidi ya watoto.

(b) Katika kuyashughulikkia masuala haya ya unyanyasaji na udhalilishaji wa watoto, wizara hupokea malalamiko ya aina hii kutoka kwa watoto wenyewe pamoja na familia zao. Hivyo, wizara hufanya ufuatiliaji kwa kushirikiana na maafisa wa Polisi na kuhakikisha zimefikishwa Mahakamani.

Wizara hufanya usuluhishi na ushauri nasaha kwa familia zilizotengana, wanawake na watoto walioteketezwa na walioathirika na vitendo vya kudhalilisha. Wizara pia hutoa ushauri wa kufuata utaratibu wa kisheria kwa watoto na familia za watoto wanaowasilisha malalamiko yao wizarani.

Mhe. Spika, wizara vile vile hushirikiana na taasisi nyengine za kisheria, kama vile Jumuiya ya Wanasheria Wanawake

(*ZAFELA*) na Kituo cha Huduma za Kisheria, kwa ajili ya kupata msaada wa kisheria na kuhakikisha haki inapatikana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza kama ifuatavyo:

Amekiri kwamba bado udhalilishaji wa watoto upo na taasisi pamoja na wizara yake inachukua jitihada kubwa. Lakini bado baadhi ya wazazi wanawatumia watoto kwa kuwapa biashara ndogo ndogo hapa mjini na mashamba kama vile kupara samaki na kuwavunjia masomo yao. Je, katika hili anasaidia vipi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa yeye kutambua kwamba serikali yetu kupitia Wizara ya Kazi imefanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo hilo.

Vile vile, nakiri pia tatizo la watoto kupara samaki pamoja na kupewa maandazi bado lipo. Lakini wizara imechukua taratibu maana miradi mikubwa, ambao ulishughulikia watoto kuwatoa katika mazingira haya ya utumikishwaji na kuwarudisha maskuli katika kijiji ya Mkokotoni.

Kwa kweli zoezi hilo la kupambana na ajira za watoto bado linaendelea na tunapata misaada kupitia Shirika la Kazi Duniani na tunakabiliana nalo ipasavyo, wala Mhe. Mjumbe asitie wasi wasi, naona kwamba suala hili tutalimudu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Tafiti za kitaalamu zinaonesha kwamba wimbi la ubakaji wa watoto linatokana na udhaifu wa sheria pamoja na utoaji wa haki. Kwa kuwa Haki za Binadamu zikiwemo Haki za Mtoto.

Je, Mhe. Waziri hivi sasa utakuwa tayari kuweka sheria maalum ya kuwahasi wale wanaofanya vitendo hivi *(Kicheko/Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, napenda kukiri kwamba tatizo la wanaofanya vitendo kama hivi linatokana na kichwa, yaani ugonjwa wa kichwa au *mental sick*, kwa sababu mtu mwenye akili yake hawezi kufanya mambo kama haya. Lakini hiyo sheria ambayo tutakayoandaa itakuwa na meno zaidi ya kuwabana hawa.

Kwa hivyo, hilo unalolitaka wewe Mhe. Mjumbe itakuwa nakiuka Haki za Binadamu na unanitafutia ubaya kwa jamii na wala siwezi *(Kicheko/Makofi)*.

Nam. 11

Ujenzi wa Bandari Ndogo Nungwi

Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:-

Gati ni huduma muhimu sana kwa usafiri na harakati za biashara katika visiwa vyetu, Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri, huoni kwamba umefika wakati ijengwe bandari ndogo huko Nungwi, ili kurahisisha usafiri na harakati za biashara kati ya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 11 kama ifuatavyo:

Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa huduma za gati katika visiwa vyetu ni muhimu sana, kwa kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa mbali mbali. Hata hivyo, wazo lake la kujenga gati huko Nungwi kwa sasa ni jambo gumu, kwa vile ujenzi wa gati ni uwekezaji mkubwa unaohitaji fedha nyingi.

Kwa hivyo, eneo hilo tayari lina bandari inayotambulika kisheria Mkokotoni, ambayo inatosheleza kwa wakaazi walioko huko. Wizara yangu haina sababu ya kujenga gati nyengine katika eneo hilo ili kuepusha matumizi mabaya ya rasilimali za serikali.

Aidha ni vigumu kujenga gati katika kila eneo la visiwa vyetu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, hivi sasa limejitokeza tatizo la watu wa Kizimkazi wenye zile boti ndogo ndogo kusafirisha abiria kutoka Kizimkazi mpaka Bagamoyo. Je, haoni kama kuna haja ya kujengwa gati hapo Kizimkazi ili kuondoa tatizo la usafirishaji haramu wa abiria.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, Zanzibar tunazo bandari tano ambazo zinatambulika kisheria. Kati ya hizo tatu zipo Pemba ambazo ni Wete, Chake Chake Wesha na Mkoani, kwa upande wa Unguja ni Bandari ya Malindi na Mkokotoni Mkoa wa Maskazini Unguja.

Kwa kweli nchi yetu imezungukwa na bahari sehemu zote yaani ni visiwa. Kwa hivyo, si rahisi kila eneo kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kujenga gati. Kwa upande wa Kizimkazi pamoja na sehemu nyengine za Mkoa wa Kusini Unguja, pengine watu wanasafirishwa bila ya utaratibu ni jukumu la Afisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba watu wao hawasafirishwi kwa njia ambazo ni kinyume na utaratibu.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mkuu wa Mkoa atusaidie ili wananchi wafuate utaratibu. Hivyo, kwa sasa serikali haiwezi kujenga gati katika eneo la Kizimkazi *(Makofi)*.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu lake Mhe. Waziri alisema kuwa Zanzibar tunazo gati tano na gati hizi tukiangalia katika kipindi kilichopita isipokuwa hii ya Mkokotoni, lakini nyengine nne kila mmoja ilikuwa na mpango wa kuongezwa, yaani kupanuliwa sehemu ili kuweza kutoa huduma kwa ufanizi zaidi.

Kwa mfano kulikuwa na mpango wa kuongezwa urefu wa gati ya Wete, Chake Chake pamoja na eneo kwenye Bandari ya Mkoani, lakini mpaka leo bado hatujaona ishara yoyote ya kazi hiyo kufanywa. Mhe. Spika, wakati watu pamoja na biashara zinaongezeka na hizi ndio njia kuu za uchumi.

Kwa hivyo, sijui Mhe. Waziri anao mpango gani wa kuona kuwa hizi bandari zetu tulizonazo zimezidishwa ili ziweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Shirika la Bandari linao mpango wa kuendeleza bandari zote.

Isipokuwa napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza kwa ujumla, kwamba tumeshafanya kwa Bandari ya Wete na Wesha suala hilo, pengine Mhe. Mjumbe hajapata fursa ya kutembelea kwenye bandari hizo, lakini kwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wameona juhudi zilizochukuliwa na Shirika la Bandari.

Kwa upande wa Mkoani sio kuongeza sehemu ya mbele, isipokuwa ni kufanya marekebisho ya bandari hiyo na zaidi ile sehemu ambayo inakabiliwa na matatizo. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu akitujaalia tunatarajia mwaka huu wa fedha Shirika la Bandari, basi marekebisho makubwa yatafanywa kwenye Bandari ya Mkoani.

Kwa maana hiyo, Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine wote ni kwamba azma ya Shirika la Bandari kuziendeleza bandari zote ipo na inafanyiwa kazi kila hali ya kifedha inaporuhusu *(Makofi)*.

Nam. 20

Ujenzi wa Viwanja vya Michezo

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, imefanya juhudi kubwa ya kuendeleza michezo nchini. Michezo ya mpira wa miguu, pete na wavu na kuleta sifa Zanzibar. Kwa sasa viwanja vya michezo vilivyo na viwango vya Kimataifa ni Uwanja wa Amani na Uwanja wa Gombani.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa viwanja hivyo havitoshi kulingana na mahitaji ya sasa.

(b) Viwanja vya Mao-Tse-Tung Unguja na Kiwanja cha Tibirinzi na Gombani ya Kale kwa Pemba vinasaidia sana Mashindano ya Kanda. Je Mhe. Waziri huoni umuhimu wa kuviimarisha viwanja hivyo visaidie kuondosha uhaba wa viwanja uliopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwepo hapa asubuhi hii tukiwa wazima wa afya. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ninaomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli kuwa viwanja vya michezo tulivyo navyo hivi sasa havitoshi kulingana na mahitaji halisi ya kukuwa kwa michezo na wanamichezo wetu kuongezeka, ambapo hivi karibuni wamekuwa wakituletea sifa nyingi Zanzibar, yaani sifa za kitaifa na kimataifa kwa mashindano mbali mbali yaliyokuwa yakifanyika.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kuwa viwanja vya Mao-Tse-Tung, Tibirinzi na Gombani ya Kale vinasaidia sana katika kuhudumia michezo yetu mbali mbali pamoja na mashindano ya madaraja ya kati na chini. Mhe. Spika, wizara yangu imeona umuhimu mkubwa wa kuviimarisha

viwanja na kuvifanya viwe bora zaidi, ili kusaidia katika mashindano mbali mbali hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, wizara yetu inafanya kila jitihada kwa kushirikiana na wahusika wa michezo kuhakikisha kuwa viwanja hivyo vinaimarishwa kwa kufanyiwa matengenezo muhimu ili viweze kutumika vizuri zaidi pamoja na kutafuta wafadhili mbali mbali, ambapo tunatarajia vitaweza kusaidia katika kufikia malengo hayo.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeze. Mara nyingi husikia kwenye vyombo vya habari kuwa wizara yetu hutafuta wahisani wapenda maendeleo kuchangia wanamichezo wanapokuwa kwenye safari za nchi za nje kwa ajili ya michezo ya kimataifa.

Je, kuna jitihada gani ambazo zinachukuliwa na serikali kwa wahisani hao kuombwa fedha kwa ajili ya kutengenezea viwanja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, wizara yetu jitihada inazochukua ni kuomba wafadhili mbali mbali. Kwa kweli hali hiyo ni kupitia serikali kuu yenyewe pamoja na kuzungumza na makampuni. Kwa mfano Uwanja wa Amani ufadhili wa pale ni kutoka serikali rafiki ya Watu wa China, ambayo ndiyo iliyotufadhili kwa ajili ya kutufanyia matengenezo Uwanja mzima wa Amani *Stadium*.

Kwa upande wa Gombani kuhusiana na masuala ya taa, *running track* pamoja na vifaa vya umeme mbali mbali ambavyo vitafungwa hivi karibuni katika uwanja ule. Kwa kweli ufadhili ule umetoka kwa Sheikh Al-Youseif kupitia jumuiya yake.

Vile vile, kiwanja cha *Tennis* kule Pemba ambacho huwa tunafanyia mashindano ya *Basketball* kwa kule Pemba pamoja na michezo mengine mbali mbali inayofanyika hapo. Kwa hiyo, ufadhili wa pale tumepata kutoka kwa Mama Shadya Karume kupitia Jumuiya yake ya *ZAYADESA*. Kwa kweli hivi karibuni tunamshukuru tena Mama Shayda Karume ametusaidia katika kiwanja kilichopo Mkoani karibu na Manispaa ambapo amekubali kutoa ufadhili wa kusaidia *(Makofi)*.

Kwa hivyo, hiyo ni mifano michache, lakini tunaendelea na mazungumzo. Pamoja na hayo, mfano mwengine ni kwa Kampuni ya *Vodacom* ambayo ilitusaidia uwanja uliopo Kikwajuni hivi karibuni wa *Handball* ambao ulianzishwa na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni pamoja na Mbunge wa jimbo hilo.

Lakini *Vodacom* nao walijitokeza kuumalizia na kuweza kufanya Mashindano ya Kimataifa ya Mchezo wa Mpiwa wa Mikono, yaani *Handball* ambayo ilifanyika hivi karibuni.

Mhe. Spika, hiyo ni mifano michache, lakini mazungumzo yanaendelea na wafadhili wa kibiashara na wengine tunaendelea kuzungumza nao.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, pamoja na juhudi kubwa ya wizara yako kuendeleza michezo mbali mbali ikiwa ni pamoja na kuvifanyia matengenezo viwanja vya Amani na Mao-Tse-Tung na vyengine. Je, unaelewa kuwa Uwanja wa Amani ambao hivi sasa unaendelea kufanyiwa matengezo makubwa na ndugu zetu wa Kichina uko katika hatari ya kuanguka kutokana na kuchimbwa kwa mchanga maeneo ya Magharibi mwa uwanja huo.

b) Kama unaelewa ni hatua zipi zinazochukuliwa ili kuinusuru hali hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa bahati nzuri hilo tatizo tunalielewa mchanga unaochimbwa ni mwingi sana kule nyuma ya Uwanja wa Amani na kweli uwanja huo uko hatarini hivi sasa tumeshaweka *fence* kwa upande wetu, lakini mchanga unachimbwa upande ule wa bondeni. Naamini sana Mhe. Mwakilishi tatizo hilo analielewa kwani tumeshafanya ziara mimi mwenyewe binafsi pamoja na Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Mjini, lakini tatizo hilo limeonekana lipo kwa Sheha wa eneo lile na Mhe. Mwakilishi anaelewa na naamini huwa wanakaa karibu sana katika kamati zao pamoja na Sheha kwa sababu kuna vibali ambavyo vinatolewa vya kuuzwa mchanga.

Pale tumeambiwa vibali hivyo vimezuiliwa, lakini bado ule mchanga unaendelea kuchotwa kwa magari ya punda na ng'ombe ifikapo nyakati za usiku. Tatizo hilo sisi kama wizara husika tayari tumeshalifikisha kwa Mkuu wa Wilaya ya Mjini na yeye alituahidi kwamba litashughulikiwa ipasavyo.

Lakini kwa kweli ni tatizo kubwa na linaweza kusababisha hatari kubwa kwa Uwanja wa Amani, naamini Mhe. Mwakilishi tutaendelea kushirikiana nae kwa vile ni eneo lake katika Shehia ile. Kwa hivyo, tunatarajia kupata masharikiano ya kutosha ili tuweze kulitatua tatizo hilo.

Nam. 52

Nyumba ya Wanafunzi Kupewa Majeshi

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mwishoni mwa mwezi Novemba 2009, baadhi ya vyombo vya habari viliripoti kuwa Wizara ya Elimu Zanzibar imetoa nyumba yake moja iliyopo karibu na Dakhalia ya wanawake *Fidel Castro* kwa Kikosi cha Jeshi la Ulinzi la Tanzania, Kambi ya Ali Khamis, Vitongoji Pemba.

(a) Je Mhe. Waziri, suala hilo ni kweli. Kama ni kweli kwanaini Wizara imefikia uamuzi huo.

(b) Kama ni kweli huoni kwamba kuwachanganya askari na wanafunzi kunaweza kuleta madhara kwa wanafunzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu haina taarifa juu ya kuripotiwa na baadhi ya vyombo vya habari katika mwezi Novemba, 2009 kuwa wizara yangu imetoa nyumba yake moja iliyopo karibu na Dakhalia ya Wanawake katika Skuli ya Sekondari ya *Fidel Castro* kwa Kikosi cha Jeshi la Ulinzi la Tanzania, Kambi ya Ali Khamis *Camp.*

(a) Mhe. Spika, suali hilo si la kweli wizara haijatoa nyumba ya walimu ya *Fidel Castro* kwa kikosi cha Jeshi la Ulinzi la Tanzania, kambi ya Ali Khamis *Camp*, Vitongoji Pemba.

(b) Mhe. Spika, kwa vile suala hilo sio kweli, wizara haina dhamira ya kuwachanganya wanafunzi na wanajeshi.

Nam. 7

Usafi wa Machinjio na Vituo vya Kuuzia Maziwa

Mhe. Asha Moh'd Hilal (Kny: Mhe. Amina Iddi Mabrouk) – Aliuliza:-

Mnamo mwezi wa Septemba 2009 Bodi ya Chakula, Dawa na Vipondozi kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Mifugo ilifanya zoezi la ukaguzi wa machinjio mabucha na sehemu zinazouzwa maziwa. Katika ukaguzi huo mambo mbali mbali yasiyoridhisha yaligundulika kama vile uchafu uliokithiri kwenye maeneo ya kufanyia shughuli hizo, uchafu wa nguo za wafanyakazi wa maeneo hayo ya kazi na maziwa yasiyochunguzwa kwa ajili ya kuhakikisha usalama wake kwa watumiaji.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa makosa mbali mbali yalijitokeza katika zoezi hilo ni watu wangapi walichukuliwa hatua kwa kuhusika na makosa hayo.

(b) Mhe. Waziri ni Vituo gani vinatumiwa kupima maziwa kabla ya kuuzwa kwa mtumiaji hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kuanzia mwezi wa Septemba, 2009, Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi ilianzisha rasmi zoezi la ukaguzi wa bidhaa za mifugo zikiwemo nyama na maziwa. Ukaguzi wa uchunguzi ambao kwa kitaalamu unaitwa *"investigative Inspection"* ulifanyika katika machinjio, maduka ya kuuzia nyama na sehemu ya kuuzia maziwa kwa upande wa Unguja. Miongoni mwa mambo yaliogundulika ni pamoja na uchafu uliokithiri, uchafu wa nguo za wafanyakazi na wafanyakazi hao kutofanya uchunguzi wa afya zao. *"Medical Check up".*

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Hatua ambazo Bodi ilizichukua ni pamoja na kuwapa elimu wahusika kwa sababu kwa kipindi kirefu bidhaa hizo zilikuwa hazikaguliwi. Pia, kuwataka kuimarisha usafi, kufanya uchunguzi wa afya zao na kujisaili kwenye Bodi kwa mujibu wa sheria. Wafanyabiashara wote ambao hawatatimiza masharti hayo ifikapo mwishoni mwa mwezi wa

Januari, 2010 watachukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kuwafungia biashara zao na kufikishwa Mahakamani.

c) Mhe. Spika, vituo ambavyo vimekuwa vikitumika kuchunguza maziwa kabla ya kuuzwa kwa mtumiaji ni Amani, Fuoni na Bububu ambapo vituo hivyo ni vya muda. Wafanyakazi wa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi hufika na kuchunguza maziwa katika sehemu hizo kisha huondoka. Hata hivyo, Bodi ya Chakula kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Mifugo hivi karibuni inatarajia kufungua vituo vya kudumu vya kuchunguza maziwa hapa Unguja kama ifuatavyo:-

MARUHUBI	Kwa ajili ya Wananchi kutoka Kaskazini.
AMANI	Kwa ajili ya Wananchi kutoka Wilaya ya Kati.
FUONI	Kwa ajili ya Wananchi wa Kusini.
MOMBASA	Kwa Wananchi wa Wilaya ya Magharibi.

Bodi inaendelea kufanya mipango ya uchunguzi wa bidhaa hizo kisiwani Pemba.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mabekari mengi yetu vibati vyao vina kutu na vinasababisha maradhi ya matumbo na matatizo mengine mbali mbali. Je, ana mpango gani wa bekari hizi kuchukua hatua ya kuzipitia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, nataka kusema kuwa hii bodi imeanza kufanya shughuli zake katika sehemu hizo ambazo tumezitaja. Kwa hivyo, madhali tunahisi kuna haja kupitia kwenye mabekari kuangalia vibati ambavyo vina kutu basi bodi hiyo itafanya kazi hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, huko nyuma kulikuwa na kitengo kinaitwa Kitengo cha Afya ya Jamii na kilikuwa kikifanya uchunguzi kama huo na kazi yao ikisikilizwa. Je, kitengo hiki wakipita katika maeneo hayo kuna vikwazo ambavyo wanapata kutokana na jumuiya nyengine au kazi yao inafanikisha kwa kuwa wao wana uwezo wa kuchukua hatua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kitengo hicho sasa kimefutwa ndio maana kumeanzishwa hii sheria ya chakula, dawa na vipodozi. Kwa hivyo, kazi iliyokuwa ikifanywa na hiki Kitengo cha Afya ya Jamii sasa inafanywa na hii Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Nam. 71

Mfuko wa Barabara

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Jukumu la Mfuko wa Barabara ni kuweka utaratibu mzuri na wakuaminika wa utunzaji wa fedha kwa ajili ya kufanyia matengenezo barabara. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 mfuko ulilenga kupokea makusanyo ya jumla ya Tsh. 4.703 Bilioni kwa kazi za matengenezo ya barabara hadi kufikia October 2009, jumla ya Tsh. 1.520 Bilioni zilikusanywa sawa na asilimia 32 tu ya Makadirio, Unguja na Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri, kwa kuwa hivi sasa ni nusu mwaka na makusanyo ni asilimia 31 tu, tatizo ni nini.

(b) Kwa mwaka huu wa fedha kila lita moja ya mafuta inachangia kiasi gani katika mfuko wa barabara.

(c) Kwa mwaka wa fedha unaoendelea kazi ya matengenezo ya barabara kwa kutumia *program* ya Mfuko imefikia asilimia ngapi ya utekelezaji.

(d) Vigezo gani vinatumika kuteua barabara zinazofaa kufanyiwa matengenezo kwa fedha za Mfuko.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 lenye vifungu (a),(b),(c) na (d) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa kweli hakuna tatizo lolote katika makusanyo ambayo yametokezea, makusanyo ya mfuko yanaendelea vizuri, pia mtiririko wa makusanyo hayo katika utoaji wa pesa hizo kwa matengenezo ya barabara nayo yanaendelea vizuri. Makusanyo yaliyotajwa na Mhe. Mwakilishi ya shilingi 1.52 ni ya kipindi cha miezi minne tu (Julai-Oktoba) sio miezi sita. Kiwango hicho ni cha kuridhisha kwani ukusanyaji wa kiwango kama hicho ukiendelea makusanyo yatafikia Tsh. 4.56 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 96.96 ya lengo la mwaka. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kuzidi makadirio kutegemea

na uingizaji wa mafuta. Makusanyo halisi hadi mwisho wa mwezi wa Disemba ni kama ifuatavyo:-

MWEZI:	**MAKUSANYO:**
Julai	Tsh. 350.3 Milioni
Agosti	Tsh. 368.5 Milioni
Septemba	Ths 401.7 Milioni
Oktoba	Tsh. 399.7 Milioni
Novemba	Tsh. 413.3 Milioni
Disemba	Tsh. 378 Milioni.

Jumla ni 2310 Milioni sawa na silimia arubani na tisa (49%).

b) Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kila lita moja ya mafuta inachangia Tsh. 100 katika Mfuko wa Barabara.

c) Kutokana na "*program*" ya matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi wa Disemba, kiasi cha asilimia 43 ya fedha zimeshalipwa kwa kazi za matengenezo ya barabara.

d) Vigezo vinavyotumika katika kuteua barabara zinazofaa kufanyiwa matengenezo kwa kutumia fedha za mfuko hadi sasa ni kama ifuatavyo:-

1. Matengenezo ya barabara kuu ambazo zimetumia fedha nyingi wakati wa ujenzi wake.

2. Umuhimu wa barabara husika katika shughuli za kiuchumi na kijamii kitaifa.

3. Hali halisi ya uharibifu wa barabara ukizingatia kifungu cha kwanza na cha pili nilichokitaja hapo awali.

4. Maelekezo ya serikali.

Vigezo hivyo hufanywa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na kupitishwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza napongeza kwa jitihada kubwa zinazofanywa,

lakini naomba nimuulize kwamba anajua hivi sasa kumezuka wimbi mara kwa mara kupotea kwa mafuta, mwenzi uliopita mafuta ya diesel yalipotea na sasa hivi mafuta ya petrol, lakini mitaani yapo yanauzwa kwa magendo.

Je, haoni utaratibu huu kwamba unapunguza pato hili na kwa kuwa sasa hivi mafuta hakuna, anawambia nini wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, haya mafuta yanapoingizwa nchini, ile jumla yote sisi katika zile kodi ndio tunakata kodi yetu maalum. Kwa hivyo, hatwendi huku kwenye reja reja tunachukulia kule kwenye jumla. Kwa hivyo, hesabu yetu sisi inakwenda vizuri na hakuna wasi wasi wowote. Kuhusu haya magendo yanayotendeka ni kweli serikali tunalijua na kwamba ni kuwa matumizi yamekuwa makubwa kwa kipindi kifupi kabisa na haya waagizaji wetu niseme kwamba walisinzia kwa sababu ni wazi kabisa kama wewe biashara yako inakwenda vizuri basi wewe ulete kwa wingi ili uuze vizuri.

Lakini tunafanya juhudi za kila pembe ili mafuta ya petroli yaweze kupatikana. Jana tulihangaika sana tupate kutoka Dar es Salaam tumepata habari kwamba hivi alfajiri imekwenda kutia nanga meli ya mafuta na matarajio yangu kwamba hivi sasa inapakia na inshaallah kama mambo yatakwenda vizuri labda mchana wa leo meli hiyo ya mafuta ya petroli inatarajiwa. Pia, mipango mengine ilikuwa meli ya Zanzibar Petrolium tayari iko Mombasa nayo ilikuwa iingie kwenye bandari kupakia, lakini wenyewe Kenya nao wana *shortage* wakasema wameishiwa wakasema kwanza mtu kwao.

Kwa hivyo, tumeambiwa tusubiri siku nne kwa huko Kenya. Nafikiri mambo yakenda vizuri naamini pengine mwisho wa wiki hii mapema wiki ijayo tatizo hili litaondoka. Zaidi tunawabana hawa wawekezaji kwamba kuna sheria yetu inasema wasipungue asilimia 40 katika matangi yao, tumegundua hilo hawalifuati. Kwa hivyo, tutajitahidi tusimamie vizuri tuone kwamba matatizo haya ya mara kwa mara hayapo kabisa.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b):

a) Mhe. Spika, kuhusu hawa wafanyabiashara ambao wanaleta mafuta, mimi naamini kwamba kwa taratibu zilizowekwa hawa ilikuwa wanaleta maombi yao halafu wanapewa hizo kazi. Sasa kwa *experience* ya miaka hii mitano inaonesha hizi kampuni ambazo mmezichagua hazina uzoefu wa biashara hii au hawana uwezo wa biashara hii. Kwa sababu mfanyabiashara yeyote yule anaangalia soko

lake, soko likiwa kubwa unaongeza biashara yako na tija inaongezeka. Mimi nashangazwa kuona kwamba hakuna hata mtu mmoja hapa anayekwenda *shell* akakopeshwa mafuta kila mmoja analipa pesa taslimu, vipi leo hawa jamaa wanakaa mpaka dakika hii nchi inakuwa katika hali ya madhila. Je, nataka kujua mpaka sasa unacheka nao tu au umechukua hatua gani dhidi yao kuhusu suala hili.

b) Mhe. Spika, mafuta yanapokuja nani anayechunguza *quality* ya mafuta hayo. Ni kwamba tuna matatizo ya mafuta yanayokuja sasa hivi ni machafu na ya kiwango cha chini kabisa. Kwa hivyo, kuna kitengo gani kwamba mafuta yale ni salama kwenye magari yetu. Ni kwamba magari mengi yanayoleta hapa Zanzibar yanaharibika kutokana na *oil* inayokuja.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa utaratibu ni kuwa tumezembea kuwachukulia hatua. Ukweli ni kwamba tumeshawaandikia na taratibu za kuwapiga faini na hizo tunakwenda nazo na kama nilivyozungumza awali kuwa huu ni uzembe na sote tumeona kipindi kirefu walikuwa wanafanya vizuri sasa wenyewe wamesema kwamba matumizi yametokea ghafla kuwa ni makubwa. Sasa kama matumizi yametokezea kuwa makubwa na wewe ukubali na yale matumizi yenyewe, lakini huo ni uzembe tu. Mimi nilikwenda kuzungumza na hawa wa GAPCO ananiambia meli ya Ukombozi ambayo tumekodiwa imeharibika, sasa kama imeharibika ndio ufunge mikono, imeharibika, kodi meli kwa mwenzio ulete uendeleze biashara miezi miwili sasa. Kwa hivyo, huo ni uzembe kwenye utendaji tu.

Mhe. Spika, mimi nafikiri Mhe. Mwakilishi yeye ni mfanyabiashara serikali iko huru kwamba kama unataka kuleta mafuta, wewe omba na taratibu zote kwani hatukujibainisha kwa hawa watatu kwa yeyote milango iko wazi, wewe utafuata taratibu zetu tutakupa, utaekeza mwenyewe tena nafikiri ushindani utazidi. Kwa hivyo, milango iko wazi kwa mwengine yeyote kuleta mafuta. Hilo naliweka wazi kabisa.

Mhe. Spika, juu ya *quality* ya mafuta ni kweli *observation* zake ni kweli kumekuwa na matatizo ya mafuta machafu. Lakini nataka kusema kwamba kuna Idara maalum ya nishati katika Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Nafikiri Mkurugenzi nimemuona akiingia hapa, nafikiri hili amelisikia. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako mimi na Mhe. Mansoor Yussuf Himidi tutalisimamia ipasavyo kuona kwamba mambo haya tunayadhibiti. Ahsante sana.

Nam. 97

Ugonjwa wa Majogoo ya Kisasa

Mhe. Ame Mati Wadi - Aliuliza:-

Katika jitihada za kuwainua wafugaji, Idara ya Mifugo kwenye Bajeti ya Mwaka 2008/2009, ilikuwa na lengo la kusambaza kwa wafugaji mifugo ya kisasa yenye ubora wa viwango vinavyokubalika Kimataifa. Katika juhudi hizo, kiasi cha mitamba 764 wa ng'ombe bora wa maziwa, mbuzi 1439 wa maziwa, na majogoo bora 700 wametolewa kwa wafugaji. Hiki ni kiwango kizuri sana kwa ajili ya kukuza ufugaji. Kilichobaki ni wafugaji wenyewe kuendeleza. Lakini nilipata kuwasikia baadhi ya wafugaji wa kuku kuwa majogoo hayo mengi yalipata ugonjwa na mengine walikufa.

(a) Je, Mhe. Waziri habari hii ina ukweli gani.

(b) Kama ni kweli, nini kilisababisha ugonjwa na vifo vya majogoo hayo.

(c) Wizara inawashauri nini wafugaji kuhusu utunzaji bora wa Majogoo hayo.

(d) Je, Serikali inao mpango wa kuendelea na kutoa majogoo hayo kwa wakulima zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 97 lenye vifungu (a), (b), (c), na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, majogoo yalioagiziwa na kupatiwa wafugaji ni kweli baadhi yao yamekufa na hili ni jambo la kawaida.

(b) Vifo vya majogoo hayo vimetokana na maradhi ya mahepe na kuhara damu kwa kuwa majogoo hayo hayakuwa na kinga kwa vimelea vya maradhi haya vya hapa Zanzibar na pia upungufu wa lishe bora umechangia vifo hivyo, kwani majogoo haya yanahitaji mazingira mazuri na lishe bora.

(c) Wizara imewawekea wafugaji mashamba darasa (skuli za wakulima) ambapo zimeenea sehemu nyingi ambapo wafugaji wanapatiwa taaluma ya kuwatunza kuku hawa wa makabila ya kienyeji waliotoka nje ya Zanzibar.

(d) Serikali kupitia Mradi wa *SDP-L* imetoa majogoo katika shehia 10 kwa kila Wilaya. Kwa awamu ya mwanzo zoezi hili limekamilika lakini baada ya kutathmini matokeo ya awali,wizara kupitia mradi husika itajadiliana na wahisani kuendeleza zoezi hili.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali mama amekiri kwamba baadhi ya majogoo yamekufa lakini yalikumbana na maradhi ya mahepe pamoja na kuhara damu. Lakini wizara ambayo inahusika na mafunzo na tiba kwa wafugaji hasa hao wa kuku. Je, baada ya kuona kwamba yapo mahepe na maradhi ya kuhara damu kwa kuku hao wizara yake imechukua hatua gani ya kinga na hatua gani ya tiba.

b) Baada ya kuhamasisha wafugaji ni kwamba waliitikia wito, lakini sasa hivi wafugaji hao wamebakia na makuku majike majogoo bado hawajawapelekea na yaliyopelekwa yamekufa. Je, anawashauri nini wafugaji hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, ni kweli wizara yangu inahusika na masuala haya ya tiba na kutoa taaluma na ndio maana tukasema kwamba tumeanzisha haya madarasa yapo Unguja na Pemba katika shehia kumi katika kila wilaya na ndio hapo wakulima wetu wanatakiwa wende wakajifunze. Kama tulivyosema ni kuwa imetokana na suala zima la lishe bora ambapo baadhi ya kuku wanakuwa hawapati lishe na kama unavyowajua jogoo ukishampeleka kwenye mabibi anafanya kazi ya ziada. Kwa hivyo, akikosa lishe ina maana pale na yeye anaweza kupata maradhi na anaweza kupata udhaifu hata kwa binadamu ndio hivyo hivyo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, bila shaka wizara yake iliwahamasisha wafugaji na wakawaandalia utaratibu wa kuwa na skuli za kuku na wakajitahidi kukusanya kuku mmoja mmoja kila darasa likawa lina kuku 25. Sasa hivi wamebakia kuku wake tu. Je, wizara yake ina utaratibu gani au inawaambia nini wafugaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, Wizara yangu moja katika jitihada ilizonazo ndio pale niliposema kwamba kwanza tunategemea kufanya *evaluation* kuhusiana na suala zima la mambo ya kuku pamoja na wahisani wetu na tunategemea mwezi Machi. Baada ya kujua hapo tutawaambia wafadhili wetu waweze kutusaidia fedha za ziada ili tuweze kununua kuku wa ziada kwa wakulima wetu.

Lakini pia, kupitia mradi wa *PADEP* ambao nao unatoa kuku.Kwa hivyo, tutazungumza kwa sababu bado umo ndani ya Wizara yangu ya Kilimo kuhakikisha yale maeneo ambayo yana kuku wake watupu kuweza kuwapatia majogoo kuendeleza mifugo hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, naomba niulize swali lifuatalo. Jogoo mmoja kwa kawaida anatakiwa awe na mitamba mingapi au makoo.

Lakini la pili, je, uwiyano huo ndio wanaopangiwa.

Na tatu, ikiwa uwiyano huo sio wanaopangiwa haionekani kama majogoo hawa wanafanya kazi kubwa zaidi kuliko kile kiwango chao na ndio maana wakafa. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nilisema mwanzo kwamba moja ya kinachohitajika kwanza ni lishe bora, na baada ya kuanzisha hizi skuli, darasa ndizo zenyewe ambazo zinatoa taaluma ya ziada kuweza kuona kwamba hawa kuku wanatakiwa wawe vipi. Lakini na jengine nikasema kwamba lile suala la Mwenyezi Mungu nalo haliwezi kupingika, yaani inavyotokezea maradhi ya mahepe na zaidi kwa kipindi cha joto kuku wengi hata wale tuliowazoea wa majumbani wanakuwa wanapata maradhi. Kwa hivyo, lile halizuiliki.

Lakini suala la matumizi inategemea na nguvu ya jogoo mwenyewe. Sina uhakika katika suala hili na naomba Mhe. Spika, nimjibu kwa maandishi idadi ya wale kuku ambao wanatumia jogoo mmoja. Lakini siamini kwamba labda linachangiwa na kuwapanda makoo wengi ndio maana wanakufa, hili halina uhusiano kabisa, lakini nitamjibu zaidi kwa maandishi.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwanza napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi nyengine tena kuja kusimama katika *podium* hii kutoa ufafanuzi wa hapa

na pale katika michango mbali mbali iliyotolewa na Wajumbe Waheshimiwa wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, binafsi yangu natoa maoni kwamba nimefurahishwa sana na namna mswada ulivyopokelewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na nawashukuru sana kwa hilo na inaonesha wazi kwamba nia ya kujenga kwa kweli tunayo kwa pamoja kabisa.

Mhe.Spika, Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia mswada wangu ni 16, ni vizuri niwataje ili tuweze kuwatambua mmoja baada ya mmoja kwa ukumbusho kwa sababu sote tulikuwepo katika kipindi chote hicho:

1. Mhe. Haji Omar Kheir (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala)
2. Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Kivuli Wizara ya Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora)
3. Mhe. Abubakar Khamis Bakary
4. Mhe. Ali Suleiman Ali
5. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
6. Mhe. Rashid Seif Suleiman
7. Mhe. Ali Abdalla Ali
8. Mhe. Said Ali Mbarouk
9. Mhe. Mohamed Ali Salim
10. Mhe. Juma Duni Haji
11. Mhe. Ahmed Nassor Mazrui
12. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja
13. Mhe. Haji Mkema Haji
14. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi
15. Mhe. Ali Denge Makame na
16. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. natoa shukurani kwa michango na hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe ambazo zimelenga kwenye kujenga na kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mashtaka. Nimeshasema kwamba jumla ya Waheshimiwa waliochangia ni 16, katika michango iliyotolewa kuna michango ya jumla katika kuimarisha Utawala Bora, kuna michango ya kuboresha mswada pamoja na hoja ambazo zinahitaji ufafanuzi.

Nashukuru kwa michango yote ya jumla na nitaizingatia katika utekelezaji wa kazi zetu. Katika michango ya jumla michango iliyowasilishwa ni hii ifuatayo:

1. Kuimarisha taasisi zote za usimamizi wa haki za jinai

2. Kuongeza bajeti ya afisi

3. Kutoa elimu ya uraia

4. Kuandaa semina kwa Wawakilishi kabla ya kuwasilishwa miswada ya kitaalamu

5. Kuwepo na sera ya usimamizi wa jinai

Mhe. Spika, katika kuimarisha taasisi zote za usimamizi wa sheria za jinai ni kweli kwamba kunahitajika kuimarishwa taasisi zote za usimamizi wa sheria na juhudi zimechukuliwa kutekeleza jukumu hilo. Kwa mfano tayari kumeshafanyika *study* ambayo imeangalia matatizo ya jumla ya usimamizi wa jinai na imeandaa mapendekezo ya kufanya mageuzi katika mfumo wa usimamizi wa haki ya jinai. Mpango huu wa mageuzi umegawika katika sehemu saba muhimu ambazo:

1. Uzuiaji uhalifu

2. Taafira za makosa ya jinai

3. Upelelezi wa makosa na huduma zinazohitajika katika upelelezi

4. Mfumo wa uendeshaji wa mashtaka

5. Mahkama na uendeshaji wa kesi

6. Huduma za wanafunzi ambao kwa wenzetu nje wanawaita wafungwa.

7. Hoja mtambuka

Hivi sasa mpango huo upo katika hatua ya kujadiliwa katika ngazi ya kikao cha Makatibu Wakuu ambapo baadae utapelekwa katika kikao cha Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, *UNDP* imekubali kuleta wataalamu ambao watakuja kuangalia utekelezaji wa mpango huo wa mageuzi kwa ajili ya kutoa ufadhili.

Pili ,kuongeza bajeti. Ni kweli kwa kuzingatia majukumu ya ofisi bejeti bado ni ndogo, lakini serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya afisi hii. Tunaelewa kuwa kutokana na uhaba wa bajeti ya serikali, si rahisi kufikia kiwango cha juu,

lakini serikali imekuwa ikijitahidi mwaka hadi mwaka katika kuongeza hiyo bajeti. Tunaamini kuwa kadiri majukumu ya afisi hii yanavyoongezeka na umuhimu wake kuonekana ndivyo serikali itavyoongeza bajeti.

Elimu ya uraia. Mhe. Spika, afisi imekuwa ikitoa elimu ya uraia kwa njia tofauti, kwa mfano katika kusherehekea miaka saba ya afisi, afisi imetembelea maskuli na vyuo vya elimu ya juu katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa kuona umuhimu huo wa kutoa elimu ya uraia, afisi imeandaa mpango maalum wa kuendeleza kutoa elimu hiyo maskuli na vyuoni katika mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Halikadhalika, tayari afisi imeanzisha jarida linaloitwa Shahidi ambalo linatolewa na afisi mara nne kwa mwaka. Toleo la kwanza la jarida hili limetolewa mwezi wa Oktoba 2009 na toleo la pili linategemewa kutoka mwishoni mwa mwezi huu. Jarida hili linatoa elimu mbali mbali ya sheria hususan sheria inayohusiana na masuala ya jinai. Pia, Mhe. Spika, afisi ina mpango wa kuanzisha vipindi vya kuelimisha sheria za jinai kwa njia ya redio.

Sera. Mhe. Spika, suala la sera ya afisi linashughulikiwa katika mpango wa kusimamia mageuzi katika taasisi za jinai.

Mwisho semina za Wawakilishi nakubali kuwa kuna umuhimu huo kwa Wawakilishi kupata semina katika miswada ya aina hii. Lakini kutokana na uhaba wa fedha inakuwa inashindikana kufanya hivyo. Hata hivyo, kwa kuwa ni suala linaloombwa kila mara, basi ni vizuri tutajitahidi katika miswada itakayofuata tutekeleze suala hilo. Ni vizuri Wajumbe wakaweza kuelewa tangu kwenye semina inakuwa rahisi kuja kupitisha hapa ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, kuna hoja za Mwenyekiti wa Kamati ambaye alisema kuwa marekebisho yaliyofanywa tunasema sisi kuwa yanaridhiwa, kwani ni sahihi na ni ya msingi na yote tumeyapokea.

Suala la uandishi wa miswada, hili tumeshalizungumza na litapelekwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa sababu ndiko kunakoandikwa miswada wazingatie ushauri uliotolewa juu ya suala hili.

Suala la rais kutia saini sheria zote mbili za Kiswahili na Kiingereza linachukuliwa na litawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya kufanyiwa kazi, ili kuweza kujua ni sheria ipi ambayo itafanya kazi iwapo itatokea mgongano baina ya sheria hizi mbili. Unajua wenzetu wanasheria wanapenda sana kutumia sheria za Kiingereza katika kutoa ufafanuzi na kujibu hoja mbali mbali. Kwa hivyo, itabidi Afisi ya Mwanasheria Mkuu itupe

maelekezo juu ya suala hili. Hivyo, tunampelekea suala hili pamoja na kupitia sheria ya tafsiri ya sheria Nam. 7 ya mwaka 1984.

Mhe. Spika, hoja zilizotolewa na Mhe. Waziri Kivuli nazo ni nzuri vile vile. Migongano baina ya sheria za Polisi na *DPP*. Kiufupi ni kuwa hakutokuwa na mgongano baina ya polisi na afisi ya *DPP*, maelekezo ambayo *DPP* atayatoa kwa polisi ni maelekezo ya kawaida ambayo yanafuata baada ya kupata taarifa kwa kutokea tukio na hivyo kuwataka wafanye upelelezi kama ambavyo wanatakiwa wafanye chini ya sheria yao ambayo wanaitumia.

Pia, Waziri Kivuli, anasema afisi iongeze juhudi kufikia katika Wilaya zote. Afisi tayari imeshafika katika Mahkama za Wilaya ambapo kwa kuanzia tayari kesi za Wilaya kwa Mahkama ya Mwanakwerekwe zinaendeshwa na Waendesha Mashtaka wa afisi ya *DPP*. Afisi inategemea kwa mwaka huu kwenda katika Mahkama ya Wilaya ya Mfenesini na Mwera kwa Unguja na Pemba Mahkama ya Wete na Chake Chake. Hatua hiyo inatarajiwa kukamilishwa katika Mahkama nyengine Wilaya ziliyoko Mkokotoni na Makunduchi kwa Unguja na Konde na Mkoani kwa Pemba mnamo mwaka ujao wa fedha.

Mhe. Spika, Waziri Kivuli, alitwambia suala la kuwasaidia Mahabusu. Kimsingi hizi sio kazi za afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka bali hufanywa na taasisi za kiraia kama vile *Zanzibar Legal Services Centre* na *Zanzibar Female Lawyers.*

Halafu kuna suala la kuwasafisha wahalifu. Mhe. Spika, suala la kuwahamisha wahalifu wa kigeni kutoka Zanzibar kwenda nchi nyengine halitofanyika Tanzania Bara, lakini litalazimika kufanyika Zanzibar chini ya Afisi ya *DPP* kwa vile suala la uendeshaji mashtaka sio suala la Muungano.

Semina, Tayari afisi imekuwa ikiandaa semina mara kwa mara kwa Unguja na Pemba kwa taasisi mbali mbali kama Polisi, Masheha na Waandishi wa habari. Jitihada zitafanyika kufanya semina katika taasisi nyengine. Tunalichukua hili Mhe. Spika, kama alivyolileta Waziri Kivuli.

Consultative meeting. Mhe. Spika, hiki sio chombo cha afisi ya *DPP* bali ni chombo kilichowekwa kwa ajili ya kurahisisha uendeshaji wa kesi. Kazi yake ni kujadili matatizo yanayojitokeza na namna ya kuyatatua. Mahkama kama ndio hatma ya suala la haki ndio mdau mkubwa, Uongozi wa Mahkama uko wa aina mbili, wa kusimamia kesi na wa mambo ya utawala. Kwa mfano masuala ya ufuatiliaji wa mashahidi hayamhusu jaji bali yanamhusu mrajis wa Mahkama, Mahkama ina nafasi mbili kwa sababu jaji hata kama ni *junior*, lakini utaratibu ni kuwa nafasi yake kama jaji yeye ana nafasi ya juu.

Mhe. Spika, hii wataalamu wamenambia kwamba jaji hata kama ndio kwanza amekuwa *appointed* na ameanza kazi lakini mnapokutana ndani ya Mahkama yeye anakuwa ndio bosi pale. Kwa hivyo, hata kama wakili amesoma kiasi gani, lakini pale bosi anakuwa ni yule jaji kwa sababu ndiye anayeendesha kesi. Hizo ndio kanuni zao. Sekretarieti ya kamati hii ni afisi ya *DPP* na Katibu wa kamati ni kutoka afisi ya *DPP*.*K*wa hivyo, tayari afisi ina Wajumbe wawili.

Kuna suala la marekebisho ya kifungu vya 99, 98, 101 wakati havimo katika sheria. Mhe. Spika, Mwanasheria Mkuu amefanya vifungu vilivyofanyiwa mabadilio na vile ambavyo havikufanyiwa mabadiliko katika sheria ya mwenendo wa jinai sura ya 14 na kupata toleo moja ambalo wanaliita *consolidated version* ambayo ndio inayotumika sasa na sio ile ambayo Wajumbe wamekuwanayo hapa na wamekuwa wakiisoma na kuifanyia *reference*. Majumuisho hayo ameyafanya kupitia kifungu cha 2(3) cha sheria Nam. 7 ya 2004 ambayo ndio iliyopitisha maudhui hayo.

Katika kifungu hicho imetoa uwezo wa kuvikusanya pamoja vifungu vyote ambavyo havikurekebishwa na sheria hii na vile ambavyo vimerekebishwa viwe katika toleo moja.Pia, katika utaratibu wametoa fursa ya kuvipanga upya kwa mujibu itakavyohitajika. Kutokana na mpangilio huo ndio vitapatikana vifungu vyengine ambavyo iwe cha 96 katika sheria hii Mhe. Spika, ndio kifungu cha 10 na kile cha 98 katika sheria hii ndio kifungu cha 11.

Katika hiyo *Criminal Procedure Act No. 7* ya mwaka 2004 inayotumika hiki kifungu cha 101 kimo na kwa sheria hii ambayo tumeijadili leo ni kifungu cha 15. vifungu hivyo vya 96, 98 na 101 ambavyo vimo katika ile sheria ndio vinafutwa na badala yake vinatumika hivi vya kifungu cha 10, 11 na 15 ambavyo vimeboreshwa.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary, alitoa michango mizuri na kwa kweli itaisaidia sana afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka katika kufanya kazi zake. Mhe. Spika, kifungu cha 56(a) kifungu hiki cha Katiba kimeanzisha nafasi ya *DPP* kama kiongo wa uendeshaji mashtaka na sio afisi ya *DPP* na ndio maana tumeleta mswada huu sasa hivi kwa kuanzisha rasmi kisheria afisi ya *DPP*. Mswada huu ndio unaoanzisha afisi ya *DPP*.

Halafu ameuliza suala la tafsiri ya *State Attorney*. Mhe. Spika, katika mswada huu *State Attorney* waliokusudiwa kwenye sheria ni wale wanaofanya kazi katika afisi ya *DPP*, tunajua kwamba wako *State Attorney* wengi kabisa. Kwa hivyo, haikuchukuliwa tafsiri ya jumla imechukuliwa tafsiri ya sheria hii.

State Attorney wa afisi ya Mwanasheria Mkuu tangu kuanzishwa nafasi ya *DPP State Attorney* hao sio sasa *Public Prosecutors*, *prosecutors* ni wale waliopata idhini ya *DPP*. Hivi sasa ma-*prosecutors* wote wanachukua idhini kutoka kwa DPP na wanapewa kibali cha kufanya kazi hiyo. Kwa hivyo, wale ni wanasheria wa serikali wanaisaidia serikali katika mambo mbali mbali.

Afisi imepewa hadhi ya *agency* kama taasisi, sio kama *agency* na *principle*, kilichokusudiwa ni muundo wa taasisi ambao uko juu kidogo kuliko taasisi nyengine. Haiwezi kuwa *agency* kwa maana iliyotajwa na Mheshimiwa kwani afisi imepewa uhuru wake chini ya Katiba. Na sio idara ile wala sio shirika. Hivyo, wamependelea watumie neno *agency*. Ni masuala wenyewe watu wa sheria wanayafahamu zaidi.

Consultancy iliyokusudiwa hapa sio binafsi, *consultancy* iliyiokusudiwa hapa ni ya kukuza sera ya jinai. Kwa mfano kuandaa sera ya watoto ya jinai kwa vile afisi ina wataalamu tofauti, basi wataalamu wa afisi hii wanaweza kufanya *consultancy* katika kutayarisha sera hiyo. *Consultancy* hii itafanywa chini ya kifungu cha 22 cha sheria.

Appointment ya *Advocate* ambaye ni mgeni au wa *private*. Yeye kwa mujibu wa sheria hii *advocate* huyu atakuwa *appointed* kwa kumsaidia *DPP* katika kuendesha mashtaka. Kiufupi *DPP* ndiye aliyeomba *service* ya *advocate* huyo na hivyo hawezi kuwajibika kulipa kama advocate wengine.

Hoja ya saba iliyotolewa na Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni kifungu cha 16 kinachoangaliwa hapa ni mambo mawili, katika kushtaki kinachoangaliwa ni maslahi ya taifa na ushahidi, sio lazima kila mtu ashtakiwe. Uwezekano wa kumsamehe mshitakiwa mmoja ili iwezekane kupata ushahidi ambao utawezesha kumtia hatiani mhusika mwengine na maslahi yatakayopatikana kwa kuendesha kesi hiyo. Iwapo maslahi yatahisi yatapatikana kwa kumsamehe mtu huyo basi *DPP* ana mamlaka hayo.

La nane ambalo Mhe. Abubakar Khamis Bakary amelizungumza ni mikutano ya kawaida baina ya *DPP* na Waziri. Tayari imefanyika kwa sasa, kwani katika sehemu zote za kisiasa Waziri ndiye msemaji wa afisi ya *DPP*. Kwa mfano ni katika uwasilishaji wa miswada, taarifa nyengine za kikao na mikutano, hii haiathiri lolote katika uhuru wa *DPP* ilikuwa ina kile kifungu cha kwamba *DPP* atakuwa anatoa *briefing* ya maendeleo ya afisi yake kwa Mhe. Waziri. Kwa sababu Waziri ndiye anayekumbana na masuala katika maeneo mengi, yeye ndiye anayekuwa anajibu hoja hata katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, ni vizuri akapata ile *erroneous* ya kila mara juu ya mambo yanavyoendelea katika afisi ile, ndio mikutano iliyokusudiwa hapo.

Kuhusiana na maadili, hilo ni sahihi na litazingatiwa kwamba maadili yamuhusu pia Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kuhusu suala la mikutano, Mhe. spika, imetajwa katika kifungu cha 22(1) kwamba mikutano itakayofanyika na afisi ya Mkurugenzi ni inayohusu na uimarishaji wa ufanisi katika usimamizi wa mfumo wa sheria za jinai.

La mwisho, ni kuhusu adhabu kwamba haikutaja kiwango cha juu. Sheria nyingi zinataja kiwango cha chini, lakini hazitaji kiwango cha juu kwa kuhofia kupungua thamani ya pesa ambapo itafanya adhabu hiyo kuwa ndogo sana na baada ya muda na kulazimisha sheria ibadilishwe kila baada ya kipindi. Hili Mhe. Spika, hata sasa hivi tuna sheria ambazo tumezirithi zamani zinaonekana wazi, kwa sababu zamani ukikamatwa na baskeli haina taa sheria ile ukiisoma faini yako ni shilingi tano, sasa hivi shilingi tano haina thamani hata kidogo. Kwa hivyo, wanaweka kiwango cha chini kwa kukimbia hiyo kupungua thamani.

Mhe. Ali Suleiman Ali, yeye alisisitiza zaidi umuhimu wa uadilifu, haja ya kuteuliwa Mkurugenzi na umuhimu wa uajibikaji na uwazi. Aidha, alisisitiza kutolewa elimu kwa Wajumbe wa Baraza na wananchi kwa jumla.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Ali Suleiman kwa suala hili na anatuhimiza tuwe *serious* katika suala la kueneza elimu ya ufanyaji kazi wa afisi ya *DPP*.

Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, tunashukuru kwa mchango wake wa kupendekeza kuwa na mkaguzi wa ndani. Hili ni suala zuri kabisa na nakubaliana na yeye kwamba ni vizuri mkaguzi wa ndani naye tumpe umuhimu kwa sababu ndiye anayesaidia kutoa zile *indication* za uharibifu unapoanza katika zile afisi zetu.

Sera ya uendeshaji wa mashtaka iliyokusudiwa hapa Mhe. Spika, ambayo Mheshimiwa ameitaja ni *prosecution policy* ambayo ni *guide line* za ndani za kuwaongoza Waendesha Mashtaka ambayo haihitaji kwenda Barazani. Hizi ni *guide line* zinakuwa ndani tu ndizo tulizokusudia katika kifungu hicho.

Halafu tatu napenda kuwahakikishia kwamba wanasiasa wanaheshimika sana, mimi mwenyewe ni mwanasiasa. Kilichokusudiwa hapa ni *integrity*. Tumepata hilo tatizo la kutafuta neno sahihi, lakini hapa Mhe. Spika, ieleweke kwamba kuna mambo mazuri, lakini kuna watu katika baadhi ya nyadhifa na kazi wanazozifanya mambo yale mazuri huwa kama kuyafanya ni kosa.

Kutabasamu ni jambo zuri na linavutia, lakini hutakiwi kutabasamu wakati wa kuswali, inakuwa umeshaharibu swala yako hapo, lakini ni suala zuri sana na linapendelewa sana.

Sasa na katika suala la kuwa wewe ni Mkurugenzi wa Mashtaka siasa tunashiriki sote, lakini wewe hutakiwi kuonekana uko *bias* kwa chama fulani. Kwa hivyo, ndio mara unazuiliwa ule uanachama wako katika kipindi kile. Sasa labda hili neno tulilolitumia tu hapa kidogo limekuwa lina matatizo kwa sababu ya utajiri wa lugha yetu ya Kiswahili, lakini ilivyokusudiwa pale ni *integrity* kusema kweli Mhe. Spika.

Nafasi ya *DPP* iko chini ya Katiba na imeanzishwa na rais. Hivyo, utaratibu ni kuwa malalamiko yote ni lazima yapelekwe kwa rais, uwasilishaji wa malalamiko hayo unaweza kutungiwa kanuni naWaziri chini ya kifungu cha 25.

Mchangiaji mwengine kama nilivyotaja ni Mhe. Rashid Seif Suleiman, amezungumza mamlaka ya kuteuwa *Deputy* ambayo yapo kwa rais. Mhe. Spika, si sahihi kwa sheria hii tu Mkurugenzi kupewa mamlaka ya kumteuwa *deputy* wake, isipokuwa yale mamlaka ambayo kisheria yapo kwa Mkurugenzi tu haya ni lazima *deputy* akasimiwe na *DPP* mwenyewe.

Mhe. Spika, mambo haya tunayafanya sana katika uendeshaji wa serikali yetu unateuwa Katibu Mkuu halafu unateuwa Naibu Katibu Mkuu, lakini wote wanakwenda kuteuliwa na rais. Kitu muhimu ni kujenga maelewano na kuondoa migongano, hilo ndilo suala ambalo sote kama tunataka tuendeshe nchi yetu vizuri tuingie kwenye hiyo *good governance* tufahamu kwamba tunafanya kazi moja tu.

Baadhi ya hoja ambazo Mhe. Rashid Seif Suleiman amezitoa nimeshazijibu katika Waheshimiwa waliopita.

Mhe. Ali Abdalla Ali amezungumzia juu ya suala la uajiri unaofanywa na utumishi. Mhe. Spika, uajiri kwa kawaida katika serikali yetu unafanywa na utumishi yaani ruhusa ya kuajiri, isipokuwa usaili ndio unaosimamiwa na afisi husika na hapa usaili unasimamiwa na *DPP*. Hii ni muhimu kwa sababu *DPP* ndiye anayetathiminiwa kila baada ya miaka mitano.Hivyo, ni muhimu apate watu wazuri ambao ataweza kufanya nao kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Rashid Seif Suleiman amezungumza mafunzo yatolewe. Mafunzo yatatolewa na *training centre* ambayo itaanzishwa na afisi chini ya kifungu cha 22 cha sheria hii. Amezungumza mengine mengi kwa kuipongeza afisi na kila kitu, hayo Mhe. Spika, tunayapokea na tunamshukuru sana kwa hilo.

Mhe. Said Ali Mbarouk yeye ametoa pongezi kwa ufuatiliaji katika masuala ya kesi za jinai uhudhuriaji wake ambao anauona. Mimi nampa pongezi Mhe. Said Ali kwa ufuatiliaji wake anaoufanya katika masuala ya kesi za jinai kwa kuhudhuria Mahkamani kusikiliza kesi za jinai.

Pili, kwa kulinda *integrity* ya afisi kutokana na unyeti wa afisi yenyewe ndio maana ikawa ni muhimu *DPP* kuwa na *control* juu ya uhamishaji wa wafanyakazi wake wote wakiwemo wahasibu. Pale unapotokea ubadhirifu basi sheria na vyombo husika vipo vitafanya kazi yake ya kumchunguza na hatimaye kumchukulia hatua ipasavyo huyo *DPP* ambaye ni mbadhirifu.

Mheshimiwa amezungumza juu ya suala la *efficiency* katika afisi ya Mkemia Mkuu. Hilo Mhe. Spika, tumelipokea na ni zuri na tutawashauri wenzetu walio na Mkemia Mkuu. Unajua Utawala Bora ni *cross cut* inagusa karibu wizara zote.Kwa hivyo, sisi kazi yetu kubwa nikutoa ushauri juu ya mawizara haya mbali mbali ya mambo mbali mbali ambayo yamejichomoza.

Mhe. Mohamed Ali Salim amezungumzia juu ya uteuzi wa Naibu Mkurugenzi kwamba uwe ni wa lazima na isiwe wa hiari, kifungu cha nne cha sheria. Kifungu hicho kimewekwa kwa kuzingatia busara za Mhe. Rais ambaye atateuwa pale ambapo ataona inafaa. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kutoa fursa kuzinagtia mahitaji, kwani inaweza ikatokea kusiwe na haja ya kua na Naibu Mkurugenzi. Itapofanywa lazima itamfanya Rais kuteuwa hata kama hapana haja kwa vile tu sheria imesema.

Hoja ya pili ni Mwanasheria wa Serikali, tayari imejibiwa katika hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ni wanasheria wa afisi hii ndio wanaohusika katika sheria hii na ndio maana wakataja huduma za ushauri zigaiwe sehemu mbili kuu iwe ni bure kwa wananchi na makampuni walipe. Ushauri uliokusudiwa hapa unahusu zaidi taasisi yaani katika masuala ya kisera na kitaalamu. Ushauri mwengine wa kisheria utaendelea kutolewa bure kwa wananchi.

Waendesha mashitaka wateuliwe haraka katika ngazi za Wilaya, hoja hii tayari tumeshaijibu katika maelezo yangu ya jumla. Halafu wakili ataeteuliwa kama Muendesha Mashtaka atakuwa ni wa muda kwa kesi maalumu na sio wa kudumu.

Mhe. Spika, maelekezo atakayopewa Muendesha Mashtaka na *DPP* yatahusiana na kazi tu na sio masuala mengine kwa mujibu wa sheria hii. Sasa hapa sera ya uendeshaji mashtaka ni sera ya ndani kama nilivyojibu ile sera ya jumla itakapokuwa tayari ambapo nishasema inatayarishwa Waheshimiwa watapatiwa mafunzo na semina.

Suala la wakili katika mashtaka binafsi kiutaratibu mtu ambae amepewa uwezo wa kuendesha mashtaka binafsi anakuwa ni mlalamikaji.Hivyo, atakuwa na haki ya kuweka wakili wa kumsaidia kuendesha binafsi na si vyenginevyo.

Kuhusu wakili kuteuliwa moja kwa moja kuendesha mashtaka binafsi na *DPP* baada ya kuteuliwa na mtu aliepewa uwezo wa kuendesha mashtaka binafsi, sababu kubwa ni suala la gharama ambalo inatakiwa kiutaratibu anaeomba kuendeshewa kesi ndie anaelipa, vinginevyo itabidi *DPP* ndie alipe.

Kuhusu waathirika gani wa uhalifu watakaopewa ushauri ni waliofanyiwa vitendo vya uhalifu kwa mfano waliobakwa na wengineo. Kuhusu taarifa za mwaka zitakazotolewa na *DPP* zitapoletwa wapi?

Kawaida taarifa hizi huchapishwa na kusambazwa kwa wahusika wote zikiwemo taasisi mbali mbali na wananchi wa kawaida. Kuhusu suala la fedha kwamba ni mali au sio mali kawaida fedha ni sehemu ya mali. Lakini sheria inatenganishwa kwa sababu maslahi ya kifedha yanaweza kuwa katika namna mbali mbali kwa mfano hundi, hawala, deni na kadhalika. Kuhusu suala la utoaji dhamana kwa ujumla ambalo amelizungumza Mheshimiwa suala hilo litaimarishwa.

Mhe. Juma Duni Haji, mezungumzia suala la migongano baina ya sheria ya polisi na sheria hii. Nimejibu kule kwamba tunategemea kwamba hakutakua na mgongano. Kuhusu sheria ya polisi kama imeshaletwa Barazani kwa kuridhiwa tutalifanyia kazi kuangalia kama tayari limeshafanyika na utakuwa umetukumbusha juu ya suala hili na tutalifanyia kazi *inshaalla*.

Kuhusu uwezo wa kukamata, uwezo huu umetolewa chini ya sheria za nyendo za jinai umetolewa kwa polisi na hata raia wa kawaida isipokuwa kwa kosa kujulikana mara tu baada ya kukamatwa afikishwe polisi. Utaratibu wake umeelezwa kwa urefu katika sehemu ya tatu ya sheria hiyo. Hivyo, ni muhimu kwa wote wanaofanya hivyo ikiwemo raia, polisi na hata vikosi wafate utaratibu huo ulioelezwa. Na Ofisi inajaribu sana kuwafanyia semina watu wa vikosi na watu wengineo ili kuweka sawa kwenye suala hili.

Kuhusu mapendekezo ya mpangilio wa vifungu vya sheria kuwekwa vizuri Mhe. Spika, utazingatiwa ni vizuri na wazo zuri kabisa. Kuhusu hoja ya kuwa na naibu ameelezwa mafao yake. Lakini *DPP* hakutajwa ni kwamba mafao ya *DPP* yameelezwa chini ya Katiba katika kifungu cha 111 na tayari sheria mahususi imetungwa kwa ajili hiyo ndio maana kwenye sheria hii haikuingizwa.

Kuhusu suala la raia anapotaka kumshtaki polisi na polisi akakataa raia anaweza kupeleka malalamiko katika ngazi mbali mbali za polisi na pia anaweza kuomba mashtaka binafsi ama kufungua kesi ya madai kutegemea na suala ambalo anataka kushitaki.

Kuhusu pendekezo watendaji wote wa afisi na sio *DPP* tu wasiwe wanachama litaingizwa katika kanuni na maadili, tutatayarisha kanuni na tutaingiza masuala haya. Suala la mipaka katika upelelezi limeelezwa katika sheria ya mwenendo wa jinai kwamba ni miezi ninne kwa kesi ambazo zina dhamana na miezi tisa kwa kesi ambazo hazina dhamana.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, mchango wako kuhusu kuimarisha Mahakama, polisi na Vyuo vya Mafunzo ni hoja ya msingi na zitaendelea kushughulikiwa wakati hali itakavyoruhusu.

Pili, afisi kutokuwa huru tayari nimeshalijibu hili na umesema katika ule mswada wa Kiswahili limeandikwa vizuri zaidi kuliko ulioandikwa kule kwa sababu limetumika lile neno ajensi kama nilivyosema mwanzo wamehangaika hapa kwa kutafuta neno sahihi la kulitumia pale, lakini chombo ambacho kiko juu kuliko idara za kawaida.

Nafasi ya *DPP* kutangazwa utaratibu upo katika nafasi za uteuzi wa Rais, lakini utumishi kwa ujumla serikalini umefanyiwa mapitio na hoja hii inaweza ikazingatiwa.

Mchango kuhusu *consultative committee* kuwa kazi zake zitanuliwe zaidi kwa mujibu wa kifungu 23 (8e) kina uwezo mkubwa wa kufanya kazi nyingi zaidi kwa kamati hiyo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, hoja yake ya mwendo wa polisi katika kushughulikia kesi Mhe. Spika, inapokelewa na itafanyiwa kazi. Suala kuwa kwa nini kuwe na dhamana kwa majambazi na wabakaji si suala la matakwa ya sheria, lakini nasheria yenyewe pia nayo iko katika kufanyiwa marekebisho makubwa na hili ni jambo moja ambalo litazingatiwa na hii sheria italetwa hapa hapa Barazani Mhe. Spika, inaangaliwa hivi sasa na ofisi ya *DPP*.

Hoja ya kuwa rafiki aongezwe katika watu ambao *DPP* anawajibika kuhusu suala hili, nadhani wigo wa marafiki ni mkubwa.Hivyo, si busara kuliingiza katika sheria hata hivyo halimzuii *DPP* kwa busara zake akahisi urafiki alionao na mshitakiwa aeleze na kutanza maslahi yake na akaacha kushughulikia kesi hiyo.

Mhe. Spika, hoja ya kuwa tuhuma zinapowasilishwa kwa Rais, *DPP* asipewe taarifa bali ufanyiwe uchunguzi moja kwa moja ni muhimu tuelewe kuwa nafasi ya DPP imelindwa kikatiba. Kwa hivyo, *DPP* atoe taarifa kabla ya uchunguzi kuanza, ni utaratibu wa kisheria unaofatwa kwa nafasi zote zinazolindwa kikatiba, sio kwa DPP na pia inamuezesha Mhe. Rais kupata muda zaidi azidi kutafakari hizo tuhuma. Mchango kuhusu *"State Attorney*" apate fursa ya kujitetea kabla ya kumfukuza, kufanyika hilo ni jambo la lazima na litawekwa katika kanuni.

Mhe. Haji Mkema Haji, ametoa michango mbali mbali katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Afisi ya *DPP* na elimu ya uraia ambayo tumeyapokea na yatazingatiwa. Hoja ya kupeleka wanasheria katika Mahakama ya kadhi ni kuwa kesi zote zinazokwenda kule ni za madai na sio za jinai na Afisi za *DPP* inashughulikia kesi za jinai tu.

Kuhusu suala la uchunguzi wa vifo vya ghafla, *DPP* atafanya vipi na kwa kushirikiana na nani. Majibu ni kuwa kwa sasa hakuna sheria maalimu inayohusu vifo vya ghafla, tumekusudia kutunga sheria hii na sheria ndio itakayofafanua utaratibu wa ushiriki wa *DPP*. Sheria hii inatoa tu uwezo wa jumla kwa *DPP*.

Mchango wa adhabu kuongezwa kwa watakaokataa kutoa ushahidi hasa maafisa wa serikali, ni kwamba adhabu yake imeelezwa katika sheria za nyendo za jinai na utekelezaji wake utaimairishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchumuzi, amezungumza juu ya uteuzi wa *DPP*, kwamba iwe ni lazima kuongezwa maslahi kwa wafanyakazi na Chuo cha Mafunzo ni sehemu ya kujifunza kupata mafunzo wa waajiri wapya na vyanzo vyengime vya mapato viainishwe. Mhe. Spika, tunaupokea ushauri huu na tutaufanyia kazi *inshaalla.*

Vile vile, amerejea lile suala la kuboreshwa Ofisi ya Mwanakemia Mkuu na michango mingi aliyoitoa ni ya kupongeza kwa hatua zilizochukuliwa.

Mhe. Ali Denge Makame, amezungumza juu ya suala la kufanya upelelezi kabla ya kesi. Mhe. Spika, hili tunajitahidi sana kuona kwamba kabla ya kesi kwenda, basi upelelezi ufanywe na ukamilike. Wapelelezi wapate mafunzo kabla ya kuanza kazi ni nzuri sana Mhe. Spika, na Mahakimu kutumia vibaya uhuru wao kwa kuachia wahalifu. Hili ni suala itabidi lifanyiwe kazi katika ku-*reform* hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, ametoa pongezi kuhusu mswada huu na anaunga mkono mambo mengi yaliyotajwa katika mswada huu.

Mhe. Spika, michango hii yote ni ya maana na kama ninavyoahidi kwamba tutaifanyia kazi kwa ile ambayo inabidi tuifanyie kazi, tutajirekebisha kwa pale ambapo imetolewa hoja kwamba tujirekebishe. Inawezekana Mhe.Spika, katika michango hii kukawa kuna sehemu ambayo sikuizungumza, mtanisamehe sana Wajumbe, lakini Mhe. Spika, nimejitahidi sana kuzichukuwa hoja zote hizi na mimepata msaada mzuri sana kutoka mwa Maofisa wa Ofisi ya *DPP* na ndio nimeweza kusimama hapa na kuzungumza mambo haya.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kukubaliwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza zima ili kupitia mswada kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Sehemu Ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu cha	1	Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha	2	Kutumika
Kifungu cha	3	Tafsiri pamoja na marekebisho yake

Sehemu Ya Pili

Uanzishaji na Uendeshaji wa Afisi

Kifungu cha 4

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti wakati wa kuchangia nilizungumzia kwamba kulikuwa hakuna ulazima wa kuanzisha ofisi katika

sheria. Lakini nikajibiwa kwamba ile ni ofisi na yule alieteuliwa ni mtu katika Katiba. Sasa naomba tu Mhe. Waziri nimkubushe kifungu cha 55 cha Katiba kinachoanzisha Mwanasheria Mkuu, wala hakuna sheria inayoanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Sasa naomba nimpe taarifa hiyo tu lakini tuendelee.

Kifungu cha	4	Kuanzishwa wa Afisi
Kifungu cha	5	Muundo wa Afisi
Kifungu cha	6	Wafanyakazi wa Afisi na Marekebisho yake
Kifungu cha	7	

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sio kuwa sijaridhika na majibu ya Mhe. Waziri, nimeridhika sana. Lakini hata hivyo, ningependa ufafanuzi wa ziada tu. Hoja yangu ilikuwa katika kifungu cha 7(b), ilihusu suala la serikali kutoa mswada na ushauri kwa waathirika wa uhalifu. Sasa mimi bahati nzuri nina huruma sana na hawa wahalifu. Sasa hawa wahalifu walioko Magerezani, mimi niliwafanya kama na wao ni waathirika wa wahalifu haidhuru wao ndio waliofanya uhalifu.

Majibu ya Mhe. Waziri, akanambia kwamba watu wanaopaswa kuwasaidia kama *ZAFELA* na *NGO's* nyengine zinazoshughulika na mambo ya binaadamu na akanijibu kwamba Ofisi ya *DPP* haihusiki hata chembe na suala la kuwasaidia hawa wafungwa walioko Magerezani. Sasa naona kwamba ikiwa Ofisi ya *DPP* kwa sababu inahusika na masuala yote ya jinai na hawa wahalifu walioko Gerezani wanatokana na hayo hayo ya athari za jinai. Haoni kwamba kuna mapungufu ya kukosa kuwasaidia hawa watu ikiwa ofisi hii itakaa kujihusisha na kuwasaidia hawa kwa namna yoyote na kuwaachia *civil society*, haoni bado serikali itakuwa ina *abdicate road* yake ya *human right*.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, katika hoja nyengine nilioijibu, nilisema kwamba Ofisi ya *DPP* inafanyakazi ya kutoa elimu kwa watu mbali mbali ambao hasa ni raia na inafanya hiyo kazi. Lakini pia, kuna vyombo ambavyo vinajitolea wenyewe kwa ajili ya kusaidia wale ambao wanaingia kwenye matatizo, na hiyo ndio katika kujenga Utawala Bora, masuala ya ushiriki wa jamii kwetu sisi kimo katika masuala ya MKUZA wa 2020.

Kwa hivyo, *NGO's* hizi kwa kweli ni vizuri zinajitolea watu hao kwa kuwapa ushauri na kuwasaidia. Kuliko hii Ofisi ya *DPP* kama inaletewa kesi kutoka kule Mahakamani juu ya masuala haya ya jiani. Ofisi ya DPP inashughulikia moja kwa moja kama ni jukumu lake ile, kesi inapoletwa hasa kama mtu yuko

kule Mahakamani kapata matatizo kama anaweza kushitaki huku, kaleta huku kwa matatizo, ofisi hii ya *DPP* inashughulikia kusema kweli.Lakini sasa suala la kwamba wenyewe wana matatizo kule na wanatala wasaidiwe sasa tunazipa nafasi hizi *NGO's* kwa kazi hiyo tuijenge nchi kwa pamoja Mhe. Spika.

Mhe. Haji Faki Shaali: Nafikiri kidogo sasa kafafanua kitu tutakaribia kuelewana. Kwa sababu kuna suala kama wafungwa Mhe.Mwenyekiti, huyu yuko ndani anahitaji pengine labda rufaa au pengine kapelekwa ndani kwa kuonewa au hawa uwezo wa rufaa hata utalaamu wa kukata rufaa, mambo kama haya pengine *ZAFELA* hawajampitia, je, anaweza kuwasiliana na Ofisi ya *DPP* akapata msaada wa ushauri wa aina hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, anaweza kufanya hivyo.

Mhe. Haji Faki Shaali: Basi kwa maana hiyo, hata kama wametolewa hapa lakini ikiwa wanapata tuendelee.

Kifungu cha	7	kazi za Afisi
Kifungu cha	8	Fedha na Bajeti

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti mimi nazungumzia kifungu cha 8 (3c) kwa sababu kinahusiana sana na kifungu cha 22(2g), naomba nivizungumze kwa pamoja. Hapa fedha ambazo zitapatikana katika ofisi hii ni pamoja na huduma za ushauri na katika kifungu cha 22, kinasema ushauri huu kutoa ushauri elekezi au huduma zinazotafiti kwa taasisi yoyote iwe ya kiserikali au isiwe ya kiserikali.

Sasa suala langu lilikuwa mwanzo. Je, mtu yoyote anaweza akaomba ushauri katika ofisi hii. Lakini Mhe. Waziri alijibu kwamba kuna baadhi ya vyombo ambavyo alivitaja vya kiserikali. Sasa kama ni hivyo, ni vyombo vya kiserikali kwa nini katika kifungu cha 8 kuna fedha na bajeti ya afisi yaani vyombo vile lazima vitoe ushauri na vichukuwe ushauri kwa fedha na kama ni hivyo.Je, ndio tunavyofanya katika vyombo vya serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, suala lake nimelielewa kidogo kidogo sio sana. Lakini siku hizi vyombo vyetu mbali mbali vya serikali vinapokuwa vinatoa huduma kwa vyombo vyengine basi vinalipa. Huu utaratibu tumeuanzisha sasa hivi katika sehemu nyingi tu panapokuwa panatoa huduma kwa chombo chengine kinalipa. Kwa hivyo, hilo jambo mimi naliona kama ni la kawaida.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, sasa kama ni hivyo, suala moja atakuwa ameshalijibu.Lakini suala la pili, hii sentensi ilivyo hapa inaonesha kwamba ni taasisi za aina yoyote si kama zile Taasisi za Serikali alizozitaja. Sasa kama imekusudiwa kama ni Taasisi za Serikali basi ziandikwe humu ili kuondoa zile taasisi nyengine ambazo hazihusiki au kuondoa wasi wasi wa mtu mwengine yeyote yule ambae atakwenda kwa ushauri kwa sababu hapa hata mimi naweza kwenda kuomba ushauri na nitakuwa niko sawa kabisa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hicho kifungu anachokisoma kifungu cha ngapi Mheshimiwa nisaidie.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8 (3c) nakisoma pamoja na kifungu cha 22. Kifungu cha 8(3c) kinasema fedha zitakazopatikana na afisi kutokana na machapisho au mafunzo huduma za ushauri na shughuli nyengine zozote zinazofanywa na afisi kupitia kituo chake cha mafunzo. Kwa hivyo, hapa ni *open* huduma za ushauri zinazofanywa na kituo yaani huduma za ushauri zinazofanywa na kituo.

Lakini 22(2g), inaendelea zaidi kwamba kutoa ushauri elekezi au huduma za utafiti kwa taasisi yoyote iwe ya kiserikali au isiyo ya serikali. Kwa hivyo, hapa ni *open* kabisa kuwa chombo chochote kinaweza kikatoa ushauri mpaka mimi naweza kwenda kule kutoa ushauri. Sasa yeye alisema kwamba ni vyombo vya serikali.Kwa hivyo, viandikwe vile vyombo ambavyo vinaweza vikapata ushauri katika chombo hiki.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni mwanasheria, kile kifungu cha kwanza alichokitaja kilikuwa kinazungumzia hayo niliyokwisha kuyajibu. Kifungu cha pili, ndio kinatoa ushauri kwa mtu mwengine yoyote kwamba hiki kinatoa nafasi na kwa mtu mwengine zaidi japo vile vilivyotajwa katika serikali.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti.Kwa hivyo, anatwambia Mhe. Waziri kwamba mtu yoyote au chombo chochote kinaweza kikenda katika ofisi ya *DPP* kutaka ushauri hivyo ndivyo?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. MWenyekiti, hivyo ndivyo kuelekea kukua kwa ile ofisi kwa sababu ile ofisi itakuwa halafu inatoa ushauri katika mambo mbali mbali. Hivi sasa kwa uwezo wao ulivyo watakuwa hawana uwezo huo. Lakini bila shaka hii imeshawekwa kabisa itakavyokuwa itakuwa inatoka kabisa.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafurahi kama ni hivyo, lakini nahisi kama kutakuwa na matatizo. Labda tungempa Mhe. Waziri nafasi akashauriana na wataalamu wake. Lakini kwa chombo chochote mtu yeyote kwenda kuchukuwa ushauri Ofisi ya *DPP* hili ni tatizo. Ofisii ya *DPP* ni chombo ambacho kinahusiana na matatizo ya serikali. Sasa watu wote Unguja na Pemba watataka ushari katika ofisi ile sijui lakini kama ndivyo hivyo sawa tuendelee. Lakini kwa sababu ya kutaka kujenga hii ofisi, naomba nitoe nafasi washauriane zaidi katika suala hilo. Pengien Mhe. Waziri ashauriane na wataalamu wake, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini kimaandishi unahisi tungeandikaje ili yaendane na hayo mashauri uliyonayo.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Kimaandishi kama si watu wote ambao wanaweza kwenda kutoa ushauri huko yaani kupata ushauri huko lazima iwe *qualified* hapa lakini ikiwa ni watu wote kama alivyokusudia yeye hii inatosha. Sasa tukipata jibu lake hasa kwamba.Je, ni watu wote waliokusudia *then* au ni baadhi ya taasisi kama alivyozitaja katika majumuisho yake. Sasa kama ndio zile zilizokusudiwa, basi zile tutaziandika, lakini ikiwa ni kila mtu.Kwa hivyo, sentensi hii inatosheleza.

Mhe. Mwenyekiti: Au tunakusudia kwamba *DPP* tumpe *description* ya kuamua ni watu au kwa jambo lipi aweze kutoa ushauri tunaonaje maana tunatunga sheria hapa.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Ikiwa tunatoa *description* kwa *DPP*.Kwa hivyo, nahii sentensi pia iwe *qualified* kwamba *DPP* kwa yale mambo atahisi kwamba anawajibika kutoa ushauri. Kwa hivyo, itabidi atoe ushauri lazima tu-*qualified.* Kwa hivyo, itakuwa yeye tumeshampa *distuation* ya baadhi ya mambo mengine kuyakataa na mengine kuyakubali. Kwa sababu ikiwa hatuku-*qualified*, nikimpelekea mimi akichukuwa wazo langu akalichukuwa uzuri na halafu ukampelekea wewe akakataa. Kwa hivyo, itakuwa ni tatizo kwa *DPP* itakuwa anabagua na hicho sicho tunachokitaka. Kwa hivyo, lazima tu-*qualified.*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Ofisi ya *DPP* inashughulikia na masuala ya jinai tu. Kwa hivyo, hatoweza kwenda mtu na jambo jengine lolote atokwenda anakwenda na suala la jinai bila shaka ndio ofisi hii inavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani Waheshimwia Wajumbe hapa wengine wanatoa *room* ya kwamba jambo hili wataalamu mkaliangalie kwa pamoja na kama itakuwa ni busara kuwa DPP apate *description* basi tui-*qualified* ionekane

kwamba DPP ana *description* ya kufanya hivyo na ijitokeze hivyo. Wajumbe nafiki tunaonaje. Haya tuendelee.

Kifungu cha 8 Fedha na bajeti ya Ofisi pamoja na marekebisho yake

Sehemu Ya Tatu

Udhibiti na Utaratibu wa Uendeshaji Mashtaka

Kifungu cha 9 Kazi na Mamlaka ya Mkurugezi

Mhe:Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia niliuliza swali linalotokana na kifungu cha 9 (2c) ambacho kinampa uwezo Mkurugenzi kuielekeza polisi na taasisi nyengine yoyete ya upepelezi wa kosa la jinai.

Sasa suala nililouliza ni kwamba hawa polisi wanafanyakazi wanasheria yao iliyoundwa na jeshi la polisi na nikasema kwamba katika hii ordinance, hii nafikiri kama ni sehemu ya 4 inatoa maelekezo ya jumla ya kazi zao ikiwemo na masuala ya upelelezi na huku kwamba tunampa *powers DPP* za kutoa maelekezo na taasisi nyengine za kufanya upelelezi. Sasa ghofu yangu niliyokuwa nayo kuwa.Je, hakutakuwa na mgongano kwamba huku wanasheria yao, hili likaidhinishwa na Baraza hili, lakini kwa bahati inafanyiwa kazi na huku *DPP* anawaelekeza.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, sikuridhika na majibu kwa sababu niseme niwe wazi kabisa unajua siku moja mimi nilikwenda kuonana na Mkuu wa Mkoa wangu, sasa kuna Mkuu wa Wilaya alimpa amri *OCD* aitekeleze, lakini akakataa kuitekeleza ile amri alikuwa ni mtu wa Bara yule *OCD*.

Sasa mimi siku ile nilikwenda kwa tatizo langu jengine pale na akanizungumzia ile amri kwa bahati nzuri akanambia Mkuu wa Wilaya bwana anataka kuniweka pabaya kwa sababu ananipa amri nitekeleze. Lakini ananambia mimi nafanyakazi chini ya sheria hii na akanambia nafanya kazi chini ya sheria hii bwana John Tendwa huyu Msajili wa Vyama, hilo suala lilikuwa la kisiasa. Sasa akanambia mimi siwezi kutekeleza amri yake, ananambia wazi wazi wakati huo nikiwa ni mwakilishi na aliniamini kwamba ni mtu mzima, nitamlindia heshima yake na sijalizungumza tokea wakati huo. Nafikiri ameshastaafu huko kwao, ndio nalizungumza leo katika Baraza hili kwa sababu sikutaka kumletea matatizo mengine yoyote katika kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, nimelishuhudia hilo kwamba huku anawajibika kwa *OCD* kufuata maelezo yake, lakini na kule ananambia mimi nafanya kazi chini ya

sheria hii. Halafu ananambia nafanya kazi chini ya Bwana Tendwa, akikusudia Tendwa ni Msajili wa Vyama vya Siasa. Ndio nikatoa mfano huu kwa sababu nina mfano hai. Sasa kwa kweli Mheshimiwa ananambia kwamba hakutakuwa na mgongano, lakini nilikuwa nina mfano hai wa suala hili.

Je, Mhe. Mwenyekiti, yeye analichukulia kijumla jumla tu kwamba hayatatokezea, lakini mimi nina ushahidi huu kwamba yametokezea. Huoni kwamba hapa panahitaji utafiti zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, jibu nililolitoa kwenye suala hili ni kwamba ushauri ambao *DPP* anautoa kwa Polisi ni ushauri wa kawaida, kwa yale mambo ambayo *DPP* kwa maoni yake anaona kwamba ushahidi haujakamilika.

Lakini uchunguzi wenyewe unafanywa kwa mujibu wa sheria yao wenyewe Polisi. Sasa kama ile sheria itakuwa imemzingia huyo Afisa wa Polisi anawajibika kuambiwa na *DPP* kwamba hivyo unavyotaka wewe sasa hivi mimi nifanye kwa mujibu wa sheria hii siwezi kufanya. DPP nae ni Mwanasheria ,kwa hivyo ,wanaweza wakakubaliana kitu gani kifanyike.

Lakini kwa kweli yeye anachotoa ushauri nini kifanyike na wanafanya kwa mujibu wa kutumia ile sheria yao, sio kwamba wanafanya kwa mujibu wa kutumia sheria hii ya *DPP*. Ndivyo, wanavyoendelea na ndivyo kesi zote walivyokuwa wanaziendesha hivi sasa. Linapelekwa *file* pale wanalitazama wakiona hawakuridhika wanawaambia hebu nendeni mkalitazame tena kwa sababu kuna upungufu huu ili wapate kwenda Mahakamani katika hali nzuri.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina malumbano tuendelee.

Kifungu cha	9	Kazi na Mamlaka ya Mkurugenzi.
Kifungu cha	10	Kukasimu Madaraka.
Kifungu cha	11	

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kifungu cha 11(3) kwa nini hawa watu ambao wanateuliwa kwa shughuli maalum hatuwatozi *fee* ili ikaingie katika mfuko wa serikali.

Nina mfano kwa sababu hapa kunaweza kukawa kuna kesi ya jinai, lakini mshtakiwa akaagizishia wakili kutoka Nairobi na hiyo imeshawahi kutokea katika kesi mbali mbali au pahala pengine. Sasa anapokuja hapa hawezi

kwenda Mahakamani tu mpaka apate kibali. Sasa kibali hiki kwa nini tumpe bure au *DPP* amuidhinishe kumpa bure, kwa nini hakuna *fee* maalum kwamba kibali kile apewe baada ya kulipa ambapo ada ile itasaidia serikali. Ndio hiki kifungu cha 11 (3) ninachozungumzia.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, jibu nililolijibu hapa ilikuwa ni kwamba huyu Mkurugenzi sasa ndie anayeomba huo msaada kwa mujibu wa alivyokusudia hapa mwenyewe. Sasa kulipa itakuwa yeye na sio yule mtu.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa hivyo ndivyo, sasa pale ambapo Muendesha Mashtaka amekuja kwa niaba ya mshtakiwa kwa nini hakuna kifungu ambacho kinasema hivyo kwamba mshtakiwa anaweza kuchukua wakili kutoka pahala popote pale. Hiyo ni *right* yake na akija hapa iwe anaweza kulipa yule wakili ili kesi iendelee na hivyo ndio inavyofanywa pahala popote tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hilo ni pendekezo jengine tutalichukua tulifanyie kazi *inshaallah.*

Kifungu cha 11	Uteuzi wa Waendesha Mashtaka na Marekebisho yake.
Kifungu cha 12	Sera na muongozo wa uendeshaji mashtaka na marekebisho yake.
Kifungu cha 13	Uratibu wa upelelezi.
Kifungu cha 14	Kukasimu kazi ya uendeshaji mashtaka.
Kifungu cha 15	Mashtaka binafsi
Kifungu cha 16	

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, hapa nimesimama kwa sababu Mhe. Waziri hakunifahamu alininukuu vibaya kuhusu kifungu cha 16 (1) (a) ambacho kinaelezea kuendesha mashauri yanayohusiana na maombi ya kusafirisha washtakiwa wa nchi nyengine waliopo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, unajua mimi mara hii mchango wangu mwingi niliuelekeza katika maswali. Swali nililoliuliza hapa, maana yake *DPP* ataendesha mashauri yanayohusiana na maombi ya kusafirisha washtakiwa nje ya nchi. Nimeangalia Katiba ya Zanzibar kifungu cha 101 (3) kinaeleza kwamba “Masharti yaliyomo

katika kifungu hiki hayatazuia sheria kuweka utaratibu kwa ajili ya kupeleka nje ya Tanzania hati zilizotolewa na Mahakama za Tanzania Bara au Mahakama za Zanzibar.

Lakini sasa swali nililouliza .Je,pamoja na hapa kwamba Mahakama ya Zanzibar imepewa uhuru huo kama ilivyo Mahakama ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu wana *concurrence jurisdiction* najua. Je, hili shauri Zanzibar kwa sababu ya malumbano tuliyokuwanayo muda mfupi uliopita inawezekana vyombo vyetu hivi kufanya jambo hili bila ya kushauriana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Sasa kwa kweli swali langu lilikuja hivyo, lakini Mhe. Waziri, alinihisi kwamba labda mimi nina *interest* sana na Serikali ya Muungano kuliko ya Zanzibar. Kwa hivyo, ilikuwa naonesha tu kwamba mimi sio kwamba niliuliza vile kwa sababu napendelea zaidi Serikali ya Muungano kuliko Serikali ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusahihisha tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi nimejibu kwamba suala la kusafirisha linafanywa na Afisi ya *DPP* Zanzibar kwa wahalifu wa nje.

Kifungu cha 16 Utekelezaji wa kazi nyenginezo zinazohusiana na marekebisho yake.

Sehemu Ya Nne

Uwajibikaji wa Kazi

Kifungu cha 17 Uwazi katika maamuzi ya mashtaka na Marekebisho yake.

Kifungu cha 18 Kutumia mamlaka kwa nia njema.

Kifungu cha 19 Kanuni za maadili

.

Kifungu cha 20 Tathmini ya utendaji.

Sehemu Ya Tano

Mambo mbali mbali

Kifungu cha 21 Kinga ya Maofisa.

Kifungu cha 22 Uimarishaji wa ufanisi katika usimamizi wa mfumo wa sheria za jinai na marekebisho yake.

Kifungu cha 23

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu *composition* ya hii kamati na nikapendekeza kwamba huyu Jaji wa Mahakama asiwe Mwenyekiti na nikapendekeza Mkurugenzi wa Mashtaka. Lakini jibu lililotoka hapa ni kwamba kwa utaratibu wa kisheria jaji ndio mkubwa. Mimi nafikiri hivyo ndivyo ikiwa yule jaji yuko katika mamlaka ya Mahakama, hapa ni nje ya Mahakama. Lakini hiyo ni kuhakikisha si kweli kwamba wakati wowote anapokuwepo jaji ndio Mwenyekiti? Naomba shahidi wangu awe Katiba ya Zanzibar kifungu cha 119.

Kifungu cha 119 cha Katiba ya Zanzibar kinazungumzia Tume ya Uchaguzi. Kinasema "Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais kwa utaratibu atakaoona unafaa". Kwa hivyo, Mwenyekiti hapa si lazima awe Jaji.

Lakini kifungu (d) kuna Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu. Kwa hivyo, Jaji ni mtu ambaye anaweza akawepo katika kamati yoyote lakini si lazima awe Mwenyekiti kwa sababu ya Ujaji wake tu haiwezekani.

Ndio maana hata katika Tume yetu Mhe. Agostino Ramadhan, aliwahi kuwa Mjumbe wa Tume lakini hakuwa Mwenyekiti. Kwa hivyo, hapo mantiki tunayosema kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka ni *better candidate* kuwa Mwenyekiti katika shughuli hii kuliko Jaji wa Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo kwa nini tusiweke hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, hii bodi iliyopo hapa kusema kweli ni bodi ya kusukuma usikilizaji wa kesi. Kuondoa yale malalamiko kwamba kesi zinachelewa pale Mahakamani kusikilizwa. Sasa katika mtu anayeendesha kesi hasa ni Jaji na Majaji wenziwe pale kwenye Mahakama.

Sasa anapokuwa Mwenyekiti, pale wanaizungumza kesi fulani wanapata ushauri, *DDP* yupo pale anaeleza malalamiko yake, daktari yupo pale anaeleza malalamiko yake, Mkemia Mkuu yupo pale anaeleza malalamiko yake. Kwa hivyo, wanashauriana wafanye nini ili kesi iweze kufunguka na iweze kwenda vizuri. Sasa hii sio Bodi ya Manangement, hii ni Bodi ya Ushauri ambayo ipo pale itakuwa inakutana.

Walikuwa wakiitumia bila ya kuiweka kwenye sheria, lakini sasa hivi wameiweka kwenye sheria kwamba wawe wanakutana kuzungumza mambo yao ya kukwamua kesi, ili kesi zikwamuke zisiwe zinaganda ganda ndio maana ya bodi hii. Ndio maana wakapendekeza kwamba basi huyu Jaji wa Mahakama yeye ndio awe Mwenyekiti na *DPP* kishaona ni vizuri awe Mjumbe tu katika ile bodi wazungumze yale matatizo.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo alizozitoa ndio kabisa sikubaliani na Jaji kuwa Mwenyekiti. Kwa sababu kwa utaratibu wetu hapa wanazungumzia kesi zilizokwama.Kwa hivyo, mtuhumiwa mkubwa ni Jaji na wenzake. Sasa yeye akiwa ni Mwenyekiti atakuwa ni *bias*. Kwa hivyo, hatuwezi kumuweka Mwenyekiti ambaye ni *bias* kwa kesi. Kwa sababu ikiwa Jaji ndie anayesikiliza kesi na kesi nyingi zimekwama halafu mimi huwezi kuniweka Mwenyekiti, lazima apatikane mtu mwengine aseme kesi zetu zimekwama kwa sababu mnafanya hivi na hivi. Mhe. Mwenyekiti, hii inaniongezea *point* zaidi kwamba huyu Jaji hafai kuwa Mwenyekiti hapa.

Lakini la pili, Mhe. Mwenyekiti, *enforcement agency* hapa katika sheria hii ni *DDP*, huyu ndie anayetakiwa a-*enforce* hii sheria. Kwa hivyo, huyu ndie mwenye dhamana ya kufanya haya. Mhe. Mwenyekiti, hapa Jaji bado mimi nahisi kwa misingi hiyo na misingi niliyoielezea mwanzo hafai kuwa Mwenyekiti. Mwenyekiti lazima awe Mkurugenzi wa Mashtaka au mtu mwengine yeyote ambaye anahisi ataona anafaa kwa sababu yule atakuwa ni *neutral* kabisa.

Sasa ama awe Mkurugenzi wa Mashtaka au awe ni mtu mwengine kabisa nje ya hao wawili ambao atakuwa ni *neutral* kabisa ili suala hili liende. Mhe. Mwenyekiti, naomba jibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri hofu ya kila mmoja kujipendelea na ndio maana sasa akaleta hili wazo pengine angekuwepo mtu mwengine ambaye ni *neutral*, si Jaji ambaye hizo kesi zimekwama kwake, wala si huyu Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye ndie anayepeleka hizo kesi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ameshajenga msimamo kwamba hakubali Jaji kuwa Mwenyekiti hapa, yeye anataka *DPP* awe ndie Mwenyekiti.

TAARIFA

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, sijajenga msimamo huu ni ushauri ambao natoa. Nilisema ikiwa si *DPP* basi Mwenyekiti mwengine

yeyote ambaye atateuliwa na Rais, si lazima awe *DPP*. Huo ndio ushauri wangu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani wenyewe wa Ofisi ya *DPP* wamehisi kwamba hili ni suala la mashauriano hawakulifikisha katika hatua ambayo Mhe.Mwakilishi amelifikisha hivi sasa kusema kweli.

Kwa hivyo, mimi naona wenyewe kwa uzoefu wao wameona kwamba ni vizuri Mkurugenzi pale akawa Mjumbe wa kawaida kwa kuweza kutoa michango yake na mambo mbali mbali, kujieleza vizuri pale mbele ya Mwenyekiti na Jaji yule asikilize malalamiko ya hawa wote. Kwa sababu hawa wote huwa wanamlalamikia Jaji, Kamishna wa Vyuo vya Mafunzo, Naibu Mkurugenzi wa Upelelezi wa Jinai, Mrajis wa Mahakama Kuu, Mkemia Mkuu. Sasa hawa wafikie makubaliano kupanga namna gani kesi fulani wanaikwamua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa sina la zaidi kusema katika hili kutokana na haya mapendekezo ambayo tayari yameshaletwa katika sheria.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Waheshimiwa Wajumbe tuifanyeje hii katika kuliamua hili. Twende kwenye kupiga kura kuwa nani awe Mwenyekiti?

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani bahati nzuri anayetoa ushauri na sio msimamo ni mwanasheria ambaye tunamuamini sote. Sisi ambao pia si wanasheria nafikiri hiyo mantiki tumeiona, ikiwa anayekwamisha kesi ni Jaji halafu yeye ukamwambie ndio ahukumu hapo tena awe Mwenyekiti kwa kweli haiingii akilini.

Kwa hivyo, mimi nafikiri tuchukue hiyo *option* ya kuwepo mtu wa tatu *neutral* ambaye ataweza kuwa yeye ni Mwenyekiti, *DPP* akawa ni Mjumbe na Jaji akawa ni Mjumbe pamoja na wengine nadhani inaingia akilini zaidi. Lakini ushauri wako Mhe. Mwenyekiti, tutauheshimu.

Mhe. Mwenyekiti: Inaonekana imefurahisha hii ya mwengine asiyekuwa Jaji au *DPP*. Nyuso zinaonesha zimefurahi hivyo. Sijaona uso unaonikatalia. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nina mashaka. Unajua hapa tunayozungumza ni mambo ya sheria. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Zakiya Omar Juma, amezungumza vizuri sana. Anayozungumza Mhe. Abubakar Khamis Bakary ,yeye ni mwanasheria. Sasa hapa huyu aliyetajwa Mwenyekiti ni Jaji

wa Mahakama Kuu kabobea kwenye sheria. Sasa tuchukue mtu mwengine yeyote hana *element* ya Ujaji *what are we doing? Let's be honest.*

Mhe. Mwenyekiti, tunaweza kusema kuna *element* ya *bias*, lakini Wajumbe hapa kifungu (b), (c), kifungu (b), Mkurugenzi wa Mashtaka ndie huyo anayemuongoza. Pia, kuna Kamishna na wengine. Huyu Jaji wa Mahakama Kuu anakula kiapo kaaminiwa yaani Jaji tena atakuwa na *bias* katika *element* kama hii, basi bora tufunge Mahakama Mhe. Mwenyekiti. *Let's be very honest*, hapa tena useme tumchukue mtu mwengine yeyote, hapa ni Jaji wa Mahakama Kuu, tutazameni kwa upeo mkubwa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Tusikie maelezo ya mwisho ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani hata kidogo na Mhe. Waziri kwa sababu mtu mwengine yeyote, kwanza hii itakuwa ni *description* ya Rais. Rais siku zote tunaamini kwamba ni mtu muadilifu na atateua mtu ambaye kweli ataweza hizi shughuli na ndio tunavyokubaliana siku zote hapa. Lakini hata ukiacha hiyo, kuna Majaji wangapi wastaafu nchi hii, kuna Wanasheria wangapi wastaafu nchi hii ambao wote wamebobea kwa sheria. Kwa hivyo, kumchukua huyo ukamuweka yeye ni Mwenyekiti wa shughuli hizi, mimi nafikiri ni mtu ambaye anaweza kazi hizi kwa sababu zinahusiana na yeye. Si lazima achukuliwe Jaji wa Mahakama Kuu.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, mimi si mwanasheria ni mwalimu lakini husikia wanasheria wana *concept* ya *natural justice*, wanasema kwamba *"A man can not be a judge of his case".* Sasa kama huyu Jaji ni Mwenyekiti ndio mara nyingi analalamikiwa anachelewesha kesi, nadhani itakuwa tunatengeneza hiyo *natural justice* kwamba mtu hawezi kuwa hakimu wa kesi yake mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kumetoka maelezo hayo na kwa kweli yako wazi. Mimi nadhani tuamue ni kweli wote waliowekwa hapa wana heshima na tunategemea na uadilifu mkubwa kwa nafasi zao. Lakini kumekuwa na maelezo hayo ya kila upande kuweza kung'ang'ania tabia ya kibinadamu unajua, ni tabia ya kibinadamu.

Nitatoa mfano mmoja mdogo sana. Hapa ndani ya Baraza mimi kama Spika ninapotoa *ruling* ambayo ikawa haikupendeza Wajumbe hapa, kuna maadili inakwenda kushughulikia jambo hilo na mimi mnanitupa nje huko kwa sababu nisije nikang'ang'ania yale maamuzi.

Mimi nafikiri tungeliangalia hili Waheshimiwa Wajumbe na kwa mifano iliyotoka tukubali kwamba jambo hili la kumuweka Jaji au *DPP* kuwa ndio Mwenyekiti nadhani tuliache. Atafutwe mtu mwengine ambaye kwa kiasi kikubwa hatokuwa *bias*. Niliona mapema kwamba hili limefurahisha Waheshimiwa Wajumbe wengi.

Basi Mwenyekiti mwengine sio kati ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kifungu cha 23 Kamati ya Mashauriano na marekebisho yake.

Kifungu cha 24

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia mwanzo kusema kwamba katika kifungu hiki cha makosa haikutiwa ile *maximum* ya faini ambayo anaweza akatozwa, imewekwa tu isiyopungua shilingi milioni moja, lakini haikuwekwa na isiyozidi shilingi milioni ngapi na huo ndio utaratibu.

Lakini alipojibu akasema utaratibu ni kwamba unamuwekea Jaji ile *minimum, minimum* ndio hii iliyowekwa kwamba isiyopungua milioni moja. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba tuweke tu isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tatu kwa mfano ili ile adhabu iwe inajulikana. Vyenginevyo Jaji anaweza akatoa faini yoyote tu ile ambayo itakuwa sivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Suala la kwamba Mhe. Jaji asije akaripuka. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, mimi sababu niliitoa ambayo Waheshimiwa Wajumbe wataizingatia. Hii sheria inatumika kwa muda mrefu na fedha tunaziona zinavyoshuka thamani. Kwa kweli madhumuni ya kuwa kuna baadhi ya sheria wanakuwa hawaweki huu ukomo wa juu kwa kuepuka hilo suala la fedha kushuka thamani.

Kuna kesi hapa zilikuwa faini zake shilingi tano, leo huwezi tena ukamtoza mtu faini ya shilingi tano katika wakati huu. Lakini sasa kama zimewekekewa mpaka inabidi basi wewe usifike pahala isipokuwa umalizike kwenye shilingi ishirini na tano. Sasa umeshaweka mpaka shilingi ishirini na tano ni kidogo sana kwa wakati huu wa sasa hivi. Kwa hivyo, hii tuizingatie tu sisi tumeikusudia kwa sababu hiyo ndio maana tukaileta hivi. Sasa Waheshimiwa Wajumbe wazingatie tufanye uamuzi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, hakuna sheria iliyokuwa haiweki kiwango cha juu cha faini. Sheria hizo anazosema za shilingi tano

zinasema “fedha isiyozidi shilingi tano” kwa hivyo, hapo huwezi ukazidisha. Hata mwakani itakuwa shilingi tano, baada ya miaka ishirini itakuwa shilingi tano kwa sababu haizidi. Lakini hapa tukiweka shilingi milioni moja na isiyozidi milioni tatu, hiyo milioni tatu itapita kipindi kirefu. Kama kutakuwa na haja ya kubadilisha si kila siku tunaleta hapa *miscellaneous amendment* kwa kubadilisha hizi faini, kutoka shilingi milioni tatu sasa tunaongeza milioni saba.

Mhe. Mwenyekiti, sheria nyingi ndio zilivyo hivi kwamba unaweka *limit.* Leo Mhe. Mwenyekiti, mtu huyu amefanya kosa kuna Jaji katika Mahakama A ikamtoza shilingi milioni mbili, lakini mtu mwengine kama huyu kosa lile lile Mahakama C ikamtoza shilingi milioni kumi kwa sababu hakuna *limit* itakuwaje? Sisi tutakuwa tunatenda *justice*. Lakini ikiwa kuna *limit* milioni moja mpaka milioni tatu *atleast* Mahakama A itatoa milioni moja na nusu au itatoa milioni mbili itakuwa *within the limit.*

Lakini tukiweka hivi mmoja atatozwa milioni moja au milioni mbili, mmoja milioni nane. Atakuja Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye namchukia mimi nitamtoza milioni sabini itakuwa hakuna *logic*. Kwa hivyo, lazima kuwe na *logic* na kuwe na *maximum* ambayo anaweza akatozwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nadhani tulizingatie hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, labda aseme tu kwamba anazungumzia kifungu namba 7 cha 24 au anazungumzia kifungu namba 1. Kwa sababu huku mbele kuna kifungu namba 7 kinasema “Mtu yeyote ambaye atapatikana na hatia ya kosa chini ya kifungu cha 3, 4, 5, 6 cha kifungu hiki atapewa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu au faini isiyopungua shilingi milioni moja au vyote viwili.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia yote katika kifungu hiki cha faini. Hii kifungo ni sawa sawa kwa sababu wamesema “kisichozidi”.Kwa hivyo, tutamfunga miaka miwili, miwili na nusu au mitatu. Lakini faini ni kwamba isiyopungua shilingi milioni moja.Kwa hivyo, tunaweka hiyo kampa shilingi milioni mbili, mwengine tatu, mwengine kumi, mwengine ishirini ikitegemea uso uliopo mbele ya Jaji. Hiyo sivyo, tuweke isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano kwa mfano. Hiyo ndio utaratibu unavyofanywa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ndio tumekaa hapa tunatunga sheria na hiyo *proposal* ndio ameshaileta Mhe. Abubakar Khamis Bakary, sasa tukubali shilingi milioni tatu au milioni tano tuweke sio mbaya.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaweka kiasi gani?

Mhe. Zakiya Omar Juma: Mhe. Mwenyekiti, hofu ya Mhe. Waziri ni kupanda na kushuka kwa thamani ya hasa pesa zetu. Sasa mimi nilikuwa napendekeza katika hilo la hofu yake na kumsaidia kuiondosha na si kwa yeye tu pengine kwa sote. Basi iwekwe kiwango cha dola ambacho kitafanywa tathmini. Kwa sababu dola huwa haishuki inapanda, sasa itakuwa ile hofu ya kushuka haipo. Kwa hivyo, napendekeza shilingi milioni moja na isizidi shilingi milioni tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Tuheshimu pesa yetu. Sauti ya shilingi milioni tano naisikia kama inazungumzwa kwa wingi. Kwa hiyo, tunafanya marekebisho kwa vifungu hivyo viwili cha kwanza na cha saba kwamba faini kuanzia shilingi milioni moja isizidi milioni tano.

Kifungu cha 24 Makosa na adhabu na marekebisho yake.

Kifungu cha 25 Kanuni

Kifungu cha 26

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, wakati ninachangia pia nilichangia kifungu hiki cha 26 na nilipata mkanganyiko mimi niliposoma. Kwa sababu hii sheria namba 7 ya mwaka 2004 ni *Amendment Act* tuliletewa hapa kuirekebisha sheria ile ya *Criminal Decree chapter 14* kama sikosei. Sasa nikasema kwamba hiki kifungu cha 98 kilichotajwa hapa katika ile *amendment* tuliyoifanya mwaka 2004 kimetajwa kwamba kinafuta sheria ile ya *Criminal Decree chapter 14.* Lakini ukweli tulichokifanya hapa katika Baraza hilo na mimi nilikuwepo hatukufuta sheria tulifanya *amendment*, lakini bahati nzuri hapa kinafutwa.

Sasa nikasema kifungu cha 101 hatukioni sasa Waziri katujibu vizuri sana kwamba imekuwa *consolidated*, katika hiyo *consolidation* ndio inaonekana. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika chombo chako kikubwa kama hiki kinachotunga sheria hiyo *consolidation* haipo.Kwa hivyo, itakuwa sisi wapikaji mambo kama haya sheria hizi zikishafanyiwa *consolidation* hazipo. Mhe. Spika, ombi langu kwa Waziri hiyo *consolidation* Barazani iwepo.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, ni ombi hicho kitabu kilichofanyiwa *consolidation* tungepata, *atleast* tuwe nacho *library* kisaidie.

Kifungu cha 26 Marekebisho ya sheria na marekebisho yake.

Kifungu cha 27	Kubakishwa na masharti ya mpito na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Baraza zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na masahihisho, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mswada wa Sheria ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya 2010

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya 2010 usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na mswada katika kusomwa mara ya pili wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya pili na kupitishwa)

Mhe. Spika: Nikushukuru Mhe. Waziri, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa mashirikiano katika kutunga sheria ambazo zimeletwa mbele yetu.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Sera ya Nishati Zanzibar

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, kwa idhini yako kwanza naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kufika tukiwa katika afya njema na siha na mimi kuniwezesha kuwasilisha Sera hii ya Nishati ya Zanzibar mbele yako na mbele ya Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Pia, nichukuwe nafasi hii kwa niaba yangu kumpongeza Mhe. Juma Duni Haji na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kwa kuteuliwa kwao kuwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi. Mwenyezi Mungu atawajaalia kila la kheri katika shughuli zao.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, azma ya Sera ya Nishati ya Zanzibar kijumla ni kuanzisha mfumo uliokubalika kitaifa kwa nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa kusimamia maendeleo ya Sekta ya Nishati Zanzibar kwa maslahi ya sasa na baadae.

Haja hii ya kuanzisha kuwepo kwa sera kunatokana na sababu mbali mbali na hali halisi inayozidi kuendelea kujitokeza hapa visiwani ambayo inatoa kila ishara ya kuwepo kwa sera hiyo.

Katika mambo muhimu zaidi ni kujitokeza umaskini, uharibifu wa mazingira, matumizi mabaya ya rasilimali ya nishati ziliopo nchini, kukosekana kwa dira ya matumizi ya nishati kwa baadae, mipango isiyo endelevu ya nishati mbadala, kukosekana kwa nishati kwa maana umeme wa dharura nchini na kukosekana kwa mpango thabiti na endelevu ya utafutaji wa nishati ya mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine kumekuwa na ongezeko kubwa kwa shughuli za kimaendeleo, ongezeko ambalo limezidisha matumizi ya nishati kwa kiasi kikubwa na uharibifu wa mazingira. Wakati matumizi ya nishati ya mafuta yameongezeka kwa wastani wa asilimia 17 baina ya mwaka 2003 na 2007 inakadiriwa kuwa na wastani wa hekta 500 za misitu zinateketezwa kila mwaka hapa Zanzibar. Kwa nchi yenye ukubwa wa kilomita za mraba 2665 ni jambo linalohitaji tafakari kubwa sana kwa vile ni la hatari.

Ukuaji wa Sekta ya Utalii kwa haraka hapa Zanzibar sekta ambayo inahitaji mazingira endelevu yanayovutia kumetoa fursa kubwa zaidi ya kimaendeleo kwa wananchi wa maeneo ya mijini na vijijini na kuipa serikali asilimia kubwa ya mapato ya fedha za kigeni kuliko sekta nyengine yoyote.

Ni wazi kuwa uharibifu wa mazingira hautoweka pazuri utalii na kwa hivyo ni tishio kubwa kwa uchumi wa Zanzibar. Hata hivyo, hatua kubwa iliyofikiwa katika jitihada za kusambaza umeme hapa nchini ili kupunguza matumizi ya nishati inayotokana na misitu imesababishwa kuongezeka kwa matumizi ya umeme mara dufu baina ya mwaka 2003 na 2008. Kwa upande mwengine imesababisha kufikiwa kwa kiwango cha kikomo cha uwezo wa umeme kutoka kwenye *greed* ya kima cha *mega watts* 45 kwa vile ndio uwezo wa mkonge unaosafirisha umeme kuja hapa Zanzibar. Hili limechangia maharibiko kwa vipindi viwili tofauti sasa na hatimaye kukosekana kwa umeme hapa Zanzibar

katika vipindi viwili hivyo vya mwaka 2008 hadi 2010 na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Kwa muda wote huko nyuma Zanzibar haikuwa na sera ya nishati na kwa hivyo hapakuwa na mikakati endelevu ya kudhibiti hali ya nishati nchini wala sheria madhubuti za upana zenye kutumika kwa sekta hii, isipokuwa kwa sheria ya kuanzisha Shirika la Umeme na ile sheria ya Idara ya Nishati na Madini. Ni wazi kuwa sheria hizi mbili haziwezi kudhibiti mfumo wa nishati hapa Zanzibar na kwa hivyo kulazimika kuwepo kwa sera ya nishati ya Zanzibar ambayo itatoa uwanja mpana kuwepo taasisi, sheria na kanuni za kila eneo muhimu ambalo linastahili kwa mantiki ya kuwepo mazingira endelevu ya kudhibiti na kuimarisha sekta ya nishati hapa Zanzibar.

Yote haya na mengineyo yanalazimisha kuwepo kwa haja ya Zanzibar kuwa na sera hii ili kudhibiti na kuweka nchi hii katika mazingira endelevu ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kusawazisha makosa yaliyokuwa wakitokea kwa sekta ya nishati kama vile tulivyokuwa tukishuhudia hapo kabla.

Mhe. Spika, ni azma ya waraka huu kuuwasilisha mbele yako na mbele ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar, kwa kutoa maelezo juu ya Sera ya Nishati ya Zanzibar kwa madhumuni ya kujadiliwa kwa kina na Wajumbe wa Baraza hili, ili kupata michango yao adhimu na kupata ridhaa yao.

Mtakumbuka Waheshimiwa Wajumbe kuwa baada ya kuonekana dosari nyingi katika kusimamia sera ya nishati hapa Zanzibar, Baraza hili kwa haraka sana liliitaka wizara yangu hii kuandaa na kuwasilisha sera hiyo mbele yenu, kwa kujadiliwa na kuipa ridhaa ili taratibu za kuanza kutumia zianze mapema kabisa. Leo hii naomba kuwasilisha rasmi sera hiyo kwa ajili ya kujadiliwa na kupata ridhaa yenu, ili kupata chombo cha kutuongoza katika kusimamia mambo yetu ya nishati kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, sera hii ni matunda ya mpango maalum ambao umeshirikishwa washirika wote stahili katika zoezi zima la matayarisho yake. Ushirikishwaji huo umeanzia kwa washiriki kutoka kote nchini, ambapo makundi mbali mbali yalihusishwa katika kushiriki makongamano ambayo yalijadili hali halisi ya sekta yenyewe, changamoto ziliopo na jinsi ya kuimarisha sekta kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Maeneo muhimu yaliyojadiliwa ni pamoja na utegemezi mkubwa wa matumizi ya nishati inayotokana na misitu kwa maana ya kuni na makaa. Teknolojia dhaifu ya matumizi ya nishati hiyo, uharibifu wa mazingira kwa kukatwa miti

ovyo, njia mbadala ya kutimiza athari hiyo na matumizi ya teknolojia za kisasa katika kukabiliana na hali halisi.

Mhe. Spika, kiujumla sera hii imefafanua kwa uwazi kupitia hoja zilizoibuliwa 24, matamko yanayokabili hoja hizo yapatayo 38 na mikakati kadhaa iliyowekwa katika kutoa suluhu ya matatizo yanayoikabili Zanzibar kwa upande wa nishati. Kwa vile sera hii ni dira, basi ni wazi kabisa kuwa masuala mengi mazito ambayo yapo mbele yetu, yatapata muelekeo katika kuyashughulikia kitaifa.

Dira ya Sera ya Nishati ya Zanzibar ni kuchangia katika maendeleo mbadala ya ustawi wa jamii wa kuwa na nishati inayojitegemea ya uhakika na rahisi kwa wote. Ni dhamira ya sera hii kuwaongoza washirika wote katika kubuni mazingira mazuri ambayo yataimarisha mabadiliko ya soko la nishati na kuwezesha uanzishwaji wa vianzo vipya vya nishati na vile vya nishati mbadala na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi na usawa wa kijamii katika kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Kwa jumla mambo muhimu yafuatayo yamezingatiwa na sera hii.

1. Tathmini ya hali ya nishati nchini.

2. Sheria katika sekta ya nishati.

3. Kipindi cha mpito kutoka matumizi ya nishati ya kuni kuelekea nishati ya kisasa.

4. Uhakika, urahisi na kujitegemea kwa ugavi wa umeme ikiwa pamoja na utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

5. Utafutaji na ukuzaji wa matumizi ya vianzo vya ndani kwa ajili ya ugavi wa nishati.

6. Kuimarisha mahitaji katika sekta za kiuchumi na kupunguza umaskini.

7. Uratibu na sheria katika sekta ya nishati.

8. Masoko ya nishati na hatua za udhibiti wa nishati.

9. Kuimarisha ufanisi katika matumizi ya nishati hapa Zanzibar.

10. Uendelezaji rasilimali watu kwa usimamizi, huduma na matengenezo ya kiufundi katika sekta ya nishati.

11. Maswali mtambuka ya sera ya nishati kwa mazingira endelevu na jinsia.

12. Majukumu ya sekta mbali mbali katika utekelezaji wa sera ya nishati.

13. Usimamizi na tathmini.

Mhe. Spika, ningependa kupata ridhaa yako na ridhaa ya Waheshimiwa Wajumbe kwa jumla, ili nieleze baadhi tu kati ya mambo yaliyogusiwa na sera hii ambayo nimeyataja hapo juu, kwa vile yameelezwa kwa urefu ndani ya kitabu cha sera ya nishati. Ningeanzia na lile ambalo limechukua muda mrefu kulijadili ndani ya Baraza hili hivi karibuni, nalo ni utafutaji na ukuzaji wa matumizi ya vyanzo vya ndani vya nishati.

Mhe. Spika, vyanzo vya ndani vya nishati mbadala. Vyanzo vya nishati mbadala ni vyanzo ambavyo havitegemei nishati inayomalizika na hupunguza athari mbaya kwa mazingira ya nchi na ulimwengu kwa jumla. Vyanzo hivi ni pamoja na vyanzo ambavyo vitatumia nguvu ya upepo, jua, mawimbi ya bahari, takataka za kilimo na kadhalika. Katika kuzalisha nishati ambayo itatumia mbali ya zile ambazo tumekuwa tukizitumia kwa muda mrefu hapa nchini kama vile vinu vinavyozalisha umeme kwa kutumia IDO.

Matumizi ya nishati mbadala yameelezwa kwa urefu katika ukurasa wa 28 hadi 31 wa sera ya nishati ya Zanzibar na mikakati ya sera imetandikwa kwa uwazi kwa ajili ya utekelezaji. Serikali kwa kupitia wizara hii na hasa Shirika la Umeme, bado inafanya mawasiliano na taasisi mbali mbali juu ya kuanzisha miradi ya aina hiyo hapa Zanzibar. Kuanza kufanya kazi kwa sera hii kutatoa mwongozo mzuri wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa sekta binafsi, ambayo inategemewa sana kwa uwanja huu. Kwa sasa uwanja uko wazi kwa sekta binafsi kuekeza nishati mbali mbali mbadala kama vile jua, gesi na upepo. Mfano mzuri wa hayo ni uwekaji wa mitambo ya umeme wa jua kwa kijiji cha Umbuji kwa Unguja na baadhi ya taasisi za kibinafsi zikiwemo skuli kama ile ya Mgogoni Pemba.

Hata hivyo, vyanzo hivi kwa muda huu vinatazamiwa kuwa ni nishati saidizi *secondary energy resources*, ili kupunguza mahitaji halisi kwa vyanzo vya msingi viliopo hapa nchini mpaka hapo Zanzibar itakapopata chaguo la nishati ya uhakika na endelevu. Mikakati ya kuuendeleza uwanja huu imeelezwa katika Sera ya Nishati ya Zanzibar kwenye ukurasa wa 30 hadi 31.

Mhe. Spika, sera hii inatoa maelekezo katika suala zima la umuhimu wa kuwa na mipango endelevu ya kuwa na nyenzo za kuzalisha umeme wa dharura. Hilo

limeelezwa kwenye ukurasa wa 23 na mikakati yake, kwa vile Zanzibar haikuwa na sera hii kwa kipindi cha nyuma, basi ni wazi kuwa uwezekano wa hali ya kuyumba yumba ambayo tulikuwa tunakwenda nayo kwa muda huo ni ya kutarajiwa. Hii ni pamoja na hali iliyojitokeza hivi karibuni ya tatizo la umeme. Kwa hivyo, umuhimu wa kutekelezwa kwa sera hii kikamilifu ni jambo ambalo historia imetudhihirishia kwa matukio haya mawili ndani ya kipindi cha miaka miwili, kwa maana ya kukatika kwa umeme hapa Unguja.

Katika mipango ya kuwa na uhakika wa umeme wa kununua kutoka nje ya Zanzibar imesisitizwa kuwepo kwa makubaliano ya bei za muda mrefu pamoja na kupunguza utegemezi huo kama mikakati inavyoeleza katika ukurasa wa 24 hadi 26.

Mhe. Spika, suala la utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Suala hili limekuwa katika mjadala wa wananchi kwa muda mrefu sasa limevuta hisia za Wazanzibari. Hata hivyo, baada ya uadilifu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, suala hilo limepata muafaka baada ya wananchi wa Zanzibar kutoa tamko rasmi kupitia chombo chao cha Baraza la Wawakilishi, kwa kuiagiza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulitoa suala hilo kutoka orodha ya mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, kwa upande wa wizara yangu nayo imeanza kuchukua hatua kwa upande wake wa kutekeleza majukumu yake yaliopewa na Baraza hili tukufu, katika kusimamia suala la mafuta na gesi asilia, ikiwemo kuwasilisha katika kikao hicho sera ya nishati ikiwa ni ufunguo wa mambo yenye umuhimu wa kusimamia utawala na uendeshaji wa masuala ya mafuta na gesi asilia hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, tamko la Sera ya Nishati ya Zanzibar. Tamko la sera kuhusiana na hili kwa maana utafutaji wa mafuta na gesi asilia, ni kwa Zanzibar ianzishe mazingira yake ya kisheria na usimamizi, kwa ajili ya uchunguzi, utafutaji, uchimbaji na kuhakikisha udhibiti wote wa hifadhi ya mafuta na gesi asilia katika maeneo yake. *Territory and territorial water*, pamoja na maeneo maalum ya kiuchumi, kwa maana *economic free zones.*

Tamko la sera linasisitiza kuwa kwenye ukurasa wa 27 hadi 31. Zanzibar itaimarisha na kusimamia utafutaji, uchimbaji, uzalishaji na usambazaji wa gesi na bidhaa zote za mafuta kwa kutilia maana hali ya kimazingira, kijamii na kiuchumi. Tamko hilo linasisitiza kuhakikisha ukusanyaji wa mapato na mgao wa uwiano wa taifa na kuyatumia ili kuleta faida kwa wananchi wake.

Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kama sera hii inavyoelekeza kwenye ukurasa wa 28, ndio chombo kitakachoridhia mifumo ya mikataba yote ya

utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Mhe. Spika, hili ni jambo muhimu sana na serikali baada ya kulizingatia imeona ni busara kwa aina yoyote ya mkataba au mikataba ambayo Zanzibar itaamua kuwa nayo, au mfumo wowote ule, basi mfumo huo uridhiwe na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Hilo limeelezwa kwenye ukurasa wa 28.

Mhe. Spika, hayo ni pamoja na mikataba ya migao ya uzalishaji, kwa maana *production share agreements* na kadhalika. Tukiamua kwenda kwenye *concession agreements* au *production share agreement*, basi mfumo huo kwanza utaridhiwa na Baraza la Wawakilishi na hatimae ndio utatumika kwa kuwapa wawekezaji.

Mikakati ya sera katika kutekeleza hayo ni pamoja na kuanzisha taasisi zitakazosimamia masuala hayo na kuanzisha na kutekeleza sheria ya mafuta na gesi asilia Zanzibar na kanuni zake. Ndani ya hayo ni pamoja na kuweka mpango mkuu wa mfumo wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia na kuweka mgawano wa faida baina ya serikali na wawekezaji. Uwazi katika utekelezaji wa suala hili ni jambo lililosisitizwa kwa ajili ya ufanisi bora katika utekelezaji na ndio maana sera hii ikaainisha wazi wazi kuwa Baraza hili tukufu ndio litakalo thibitisha mifumo ya mikataba yote ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia hapa nchini.

Ni vizuri ikumbukwe kuwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar linawakilisha maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Matakwa yao katika sura ya 2 kifungu cha 9 cha Katiba ya Zanzibar inaeleza wazi kuwa mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi, ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 10(3)(4) kinaweka bayana kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itadhibiti uchumi wa nchi na itadhibiti na kuendesha sekta muhimu za kiuchumi na kwamba mfumo wa uchumi hautofanyika katika utaratibu utakaopelekea kulimbikiza kwa utajiri na njia za kuzalisha mali kwa wachache au kikundi fulani. Kutokana na hayo ni wazi kuwa mikataba mibovu, ugavi mbaya wa mapato, muongozo mbaya wa ukusanyaji na matumizi ya mapato ya mafuta na gesi asilia na kutojali wananchi ni kati ya mambo ambayo sera hii imeeleza wazi kuwa yanahitaji baraka za Baraza la Wawakilishi kwa kutoa ridhaa ya mifumo ya utekelezaji wa mambo hayo.

Mhe. Spika, mikataba mibovu na uongozi mbaya ni mambo ambayo yamezusha migogoro na vita katika nchi nyingi za hapa Afrika, ambazo zimepata baraka ya kuwa na mafuta na gesi. Mfano mzuri ni Angola, Congo Brazavile, Chad, Jamhuri ya Afrika ya Kati na nchi nyenginezo nyingi zenye migogoro ambayo kwa gharama yoyote ni lazima tuiepuke kwa kuweka wazi

kila hatua ya zoezi zima la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, kwa kuwakabidhi wananchi wenyewe kwa kupitia taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa katiba na sheria ya Zanzibar.

Mhe. Spika, sera hii imetoa suluhisho kwa hilo kwa kutoa mikakati ya kuanzishwa mfumo wa kisheria utakaozingatia misingi ya Utawala Bora, haki na uwazi katika kusimamia mifumo ya mikataba yote ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, ambayo itaridhiwa na Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar pamoja na fidia kwa wananchi na maeneo ambayo yataathirika na harakati hizo.

Vile vile, mikakati mingineyo ni pamoja na kuanzisha kwa mfuko wa mafuta *Zanzibar Petroleum Fund Development* au kama inavyojulikana kwa baadhi ya nchi *Sovereign Fund.* Nchi ambayo inaongoza sasa hivi kuwa na mfuko wa maana ni Norway ambao wana bilioni 450 dola, katika *Sovereign Fund* yao inayotokana na mafuta na gesi hasa nchi za Arabuni na nyenginezo. Kwa hivyo, tumeweka utaratibu wa kuwa na *Sovereign Fund* au mfuko kwa jina ambalo tutakubaliana kuupa mfuko huo. Dhamira yake ni kuhakikisha mgao unaostahiki na wa haki kwa wananchi wote wa Zanzibar, na kuweka mpango mkuu wa mfumo wa ugawanaji wa faida baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wawekezaji katika sekta hiyo, na kutoa mazingira bora ya uzalishaji wa biashara katika sekta hiyo.

Mhe. Spika, MKUZA imeeleza wazi kuwa ili kufanikisha malengo ya milenia ni sharti na nyenzo muhimu katika kuleta mabadiliko ya afya, elimu, huduma ya maji, kilimo na masuala ya mazingira. Hili limetolewa tamko na sera hii katika ukurasa wa 31 na 32 kwa kusisitiza uendelezaji wa nyenzo za usambazaji wa nishati uende sambamba na mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini na usaidie juhudi zilizochukuliwa na mashirika na mamlaka husika. Lengo kuu ni kuongeza kipato cha Mzanzibari na kuimarisha huduma muhimu ambazo zitamkomboa mwananchi kutoka katika hali ya umaskini.

Mhe. Spika, suala la uharibifu wa mazingira. Sababu moja kubwa ya wawakilishi wa Zanzibar kupelekea uamuzi wa kusimamia wenyewe rasilimali ya mafuta na gesi asilia ni la mazingira. Sekta ya mazingira si ya Muungano na inasimamiwa na wananchi wa Zanzibar kwa kupitia taratibu za nchi. Kwa vile sekta ya utalii ndio chanzo kikuu cha fedha za kigeni, basi ni dhahiri kuwa kutunzwa kwa mazingira ya nchi hii ni jambo ambalo halitaki mjadala. Ni wazi kuwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, unaweza kwa kiasi kikubwa kuathiri mazingira bila ya kuwepo usimamizi wa dhati.

Sera ya Nishati ya Zanzibar kuliona hilo imetoa tamko rasmi kwenye ukurasa wake wa 44 hadi 46 kuwa Zanzibar itaimarisha mazingira ya uhakika na endelevu wakati itakapopanga juu ya hatua zinazohusiana na nishati ikiwa ni pamoja na tathmini ya athari katika mipango na miradi yote ya nishati, mali na ulazima wa kufanyiwa kwa *environmental effect assessment*, kwa maana ya tathmini ya athari kwa mazingira kwa kila miradi. Napenda kuchukua nafasi hii kutaarifu kuwa Serikali ya Norway imekubali kugharamia mpango wa kutathmini mazingira kwa upeo mkubwa zaidi. Kwa maana ya *strategic environmental impact assessment* kwa Zanzibar kwa suala zima la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Kwa eneo lote husika kama ni hatua moja kubwa kwa serikali hii katika kujali uhai wa watu wake na mazingira kwa jumla.

Mhe. Spika, katika mpango huu tathmini kubwa hufanyika kwa athari kwa masuala yote muhimu yakiwemo mazingira na uhai wa viumbe, shughuli zote za kiuchumi, kijamii na mipango mingine nchini na hata kuzingatia athari kwa eneo zima kiujumla la Zanzibar na jirani ya Zanzibar. Katika mpango huu madhumuni hasa ni kutambua na kukabiliana na athari hizo zikiwemo zile za wananchi ambao watapata athari ndani ya maeneo yao, kwa kupatiwa fidia kwa kila athari itakayowagusa ikiwa ni pamoja na makaazi ya ajira. Hii ni hatua muhimu kwa vile imejali wananchi wa Zanzibar kwa jumla na sio kwa sehemu ile ambayo inatazamiwa kufanyika mradi huu.

Mhe. Spika, suala hili la kufanya tathmini ya mazingira ni agizo la Baraza hili la Wawakilishi, ambapo tulitakiwa katika mijadala yetu pamoja na mingineyo, kufanya tathmini ya kina juu ya namna wananchi watakavyoathirika katika maeneo yao na fidia kwa wale ambao wataathirika kwa maeneo ya kilimo, uvuvi na biashara. Wale wavuvi watakaoathirika kwa kutumika fukwe zao, usafiri wa baharini, maeneo ambayo wanazalia viumbe wa baharini na kadhalika. Baada ya kuwasiliana na Serikali ya Norway, wamekubali kwamba watagharamia tafiti hiyo ya kina, kwa maana *strategic environmental impact assessment* kwa Zanzibar nzima na hatimaye kuwasilisha tathmini hiyo kwetu kwa ajili ya kuijadili na kuitolea muongozo.

Mhe. Spika, suala la uendelezaji rasilimali watu kwa usimamizi, huduma na matengenezo ya kiufundi katika sekta ya nishati. Tamko la sera ya nishati katika hili kwenye ukurasa wa 42 ni kuwa Zanzibar itakuza uwezo wa maendeleo ya nishati na rasilimali watu na itatekeleza mashirikiano baina ya sekta ya nishati na nyinginezo za serikali, binafsi na jamii kwa elimu na mafunzo. Vile vile, itakuza mashirikiano na jumuiya za biashara na makampuni kwa kushiriki katika kuendeleza uwezo wa kutoa wafanyakazi waliofunzwa. Kwa kuzingatia hayo na baada ya ushauri wa Baraza hili, Wizara ya Maji,

Ujenzi, Nishati na Ardhi tayari imefanya jitihada ya kujiandaa katika uendelezaji rasilimali watu, ili kusimamia sekta ya mafuta na gesi asilia ipasavyo.

Mhe. Spika, lengo kuu ni kuwa na wataalamu wazalendo watakaosimamia utaratibu mzima wa suala la mafuta na gesi asilia hapa nchini. Hatua ya kwanza ni kutambua mahitaji, kwa maana *need assessment*, kutafuta vyuo na hatimaye kupata wafadhili pamoja na nguvu za serikali kupeleka vijana nje ya nchi kwa mafunzo. Maeneo ya kitaalamu yafuatayo yanahusika katika zoezi hili. Degree ya Kwanza ni *petroleum engineering* tunahitaji nafasi 3, *petroleum chemistry* nafasi 3, *petroleum geo. physics* nafasi 3, *petroleum inspection* nafasi 3 na *geology* nafasi 3.

Katika Degree ya Pili, tunahitaji Shahada za *petroleum law* nafasi 3, *petroleum engineering* nafasi 3, *petroleum chemistry* nafasi 3, *petroleum geology* nafasi 3, *petroleum geo. Physics* nafasi 3, *energy development engineering* nafasi 3, *petroleum management* nafasi 3 na *human resource management* nafasi 3.

Wizara hii kwa sasa inashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kukamilisha zoezi hili kama sera inavyoelekeza kushirikisha sekta husika. Kuhusiana na fadhila, nina furaha kulieleza Baraza hili tukufu, kwamba kampuni binafsi ya mafuta na gesi asilia ya *Rasilhema Tanzania limited*, imekubali kugharamia mafunzo hayo bila ya masharti, kwa maana hawataki kitu kwetu na wasitarajie kitu kwetu na Serikali ya Norway inalitafakari kulizingatia kisekta, nina amini hatimae tutafikia pahala pazuri kwa huko pia.

Kijumla sekta zote kutoka umma binafsi na jamii ya kimataifa vitashirikishwa katika hili ili ufanisi mzuri na waharaka upatikane.

Imani ya wizara hii kuwa wataalamu Wazalendo tutaendelea kuwajengea uwezo kitaalamu, hii ni jambo la msingi kwa mwelekeo wa kuwa na teknolojia endelevu hapa nchini, ili kuwezesha suala hili kusimamiwa na Wazanzibari wenyewe *(Makofi)*.

Mhe. Spika, hili nalo ni agizo la Baraza hili tukufu katika mijadala yetu mbali mbali hata kwenye kipindi cha bajeti, wizara yangu ilielekezwa kwamba tujiandae kwa kutafuta mfadhili wa kuwaandaa vijana wa Kizanzibari.

Sasa kama ulivyosema Mhe. Spika, napenda kutoa taarifa kupitia kwako kwa Baraza hili tukufu kwamba tumelifanikisha hilo, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Mhe. Waziri wenyewe ndiye mwenye kulisimamia hili *(Makofi)*.

Vile vile, katika utoaji wa taarifa tulikubaliana hapa kwamba wale ambao watapata fursa ya kwenda huko kwa ajili ya kupata taaluma hii, basi tuwe makini katika kuwachagua kwa maana iwe *inclusive*, yaani tupate watu kutoka visiwa vyote vya Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza hili tukufu, wakati nilipokuwa nikimuandikia Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, pia nilimuandikia Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa maana ya kumpa nakla ya barua hiyo, Mhe. Hamad Masoud Hamad, Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi *(Makofi)*.

Vile vile, Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na wengine ambao wanaohusika na hili, kwa ajili ya kuendeleza yale ambayo tumeahidiana kuwa na uwazi katika kusimamia masuala haya *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri leo hii Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alikuwa na watu hao, katika kupanga mikakati ya mwisho juu ya yale mahitaji ya msingi, ambayo yanahitajika kwa vijana wetu kuweza kujiunga na vyuo hivyo, basi naamini akikamilisha hayo atawapa taarifa Wajumbe wa Baraza hili tukufu ili nao waweze kumsaidia.

Pia na mimi nilipata fursa ya kuonana nao na ahadi ya safari ile ya kwenda Ras-el-Khaima kwa ajili ya kujifunza na sisi ipo pale pale. Kwa hivyo, tutaendelea kutafuta ridhaa ya serikali kwa kushirikiana na afisi yako Mhe. Spika, ili tuweze kwenda huko sisi Wajumbe wa Baraza hili tukufu na kuweza kujifunza zaidi *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa sasa tatizo moja kubwa ambalo mapema limeanza kutukabili ni pamoja na kuwa na sekta nyingi, ambazo zinasimamia Sekta hii ya Nishati. Kwa kweli hili limepelekea kusababisha ufanisi mdogo na hata migogoro katika utekelezaji na hatimaye kusababisha huduma isiyoridhisha. Mfano mzuri uliopo kwa sasa ni udhibiti wenye mashaka wa uagiziaji pamoja na usambazaji wa mafuta nchini, kwa maana ya *petrol*, *diesel* and *kerosene*.

Katika kipindi hiki cha kutokuwepo huduma ya umeme nchini. Kwa maana sasa taathira yake inaonekana wazi zaidi. Hayo yameelezwa kwenye ukurasa wa 33 hadi 38. Pamoja na hayo imetoa dira ya kuundwa kwa chombo kimoja tu, chenye kijitegemea ambacho kitadhibiti hali ya uendeshaji wa soko la nishati ya mafuta, yaani *diesel, petrol and kerosene* hapa Zanzibar kwa kutumia sheria, kanuni na taratibu zake.

Hali hii ni pamoja na kuipa serikali na jamii uwezo wa kisheria kuweza kuingilia kati mfumo wa soko hilo ili kulinda maslahi ya wananchi kwa jumla. Pamoja na hayo, kuweka mifumo ya kodi, ruzuku, motisha pamoja na kudhibiti bei.

Mhe. Spika, kwa yale niliyokuwa nikieleza awali Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa bahati nzuri baada ya kufanikisha mazungumzo yake na wafadhili hawa, tena namshukuru sana kwa kuchukua jitihada hizo. Nimearifiwa kuwa kwa mwaka 2010 tunazo nafasi kumi za masomo katika sekta hii na haya si mafanikio madogo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nakushukuru sana, mimi mwenyewe binafsi Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na nakuomba upokee pongezi za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu la Wananchi wa Zanzibar *(Makofi)*.

Mhe. Spika, na kudhibiti bei ya nishati katika soko pale panapolazimika.

Hata hivyo, hali hiyo haina maana kuwa serikali itaingilia kati soko kwa makusudi kwa madhumuni ya kuhujumu, bali itakuwa kwa nia ya kujenga na itatekeleza hayo kwa uwazi, hadhari kubwa na wakati muafaka iwapo tu pale kutakuwa na ulazima. Kwa vile serikali inaheshimu Soko Huria, basi itakuza na kuheshimu kanuni za soko hilo kwa madhumuni hayo.

Mhe. Spika, Sera ya Nishati imeweka umuhimu mkubwa wa suala hili katika jamii yetu, kwa kusisitiza matumizi bora ya nishati hata sehemu za majumbani na taasisi kwa vile ni asilimia kubwa ya wateja wa soko hili. Ili kudhibiti ugawaji wa mahitaji ya nishati nchini, sera imeweka wazi mikakati kadhaa katika kutimiza hilo, ikiwa ni pamoja na kuelimisha hatua za kuweka viwango madhubuti kwa vifaa vinavyoagizwa.

Kutumia kodi na motisha na kuimarisha mipangilio ya kifedha kupitia mifumo ya benki na taasisi binafsi nyenginezo, ili kupatikana kwa fedha katika uwekezaji wa ubora wa nishati na uzalishaji kwa kutumia nishati mbadala. Kwa mfano mzuri wa utekelezaji wa hili ni kuondoa kodi ya mapato kwa vifaa vyote vinavyotumia nguvu za jua, gesi na matungi ya taa ya umeme yanayotumia umeme mdogo, kwa ajili ya kutoa msukumo katika matumizi ya vifaa hivi hapa nchini. Kwa bahati hili limeanza kutekelezwa na wizara hii mapema mwaka jana. Hata hivyo, juhudi kubwa zinahitajika kuchukuliwa ili kufikia malengo yatakayopangwa kwa mujibu wa maelekezo ya sera.

Mhe. Spika, Sera ya Nishati na Masuala Mtambuka. Tukiacha suala la mazingira ambalo sera hii imelipa uzito mkubwa. Masuala ya maendeleo ya

nishati yameelezwa kuwa na athari tofauti kwa wanawake, wanaume na makundi yenye mahitaji maalum. Kwa hivyo, kujali na kutimiza mahitaji maalum ya makundi haya, ni mambo yaliyopewa umuhimu katika utekelezaji wa sera hii.

Pamoja na kuungwa mkono kwa sera nyenginezo na mipango yote yautekelezaji katika vita dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu na kadhalika.

Mhe. Spika, leo ni siku ya kujadili sera yetu hii kwa madhumuni na hatimaye kuwa na zana nzito ya kuitumia katika kuujenga uchumi wetu kwa kutumia rasilimali mbali mbali za nishati kwa muongozo maalum tuliouchagua. Sera hii si kwamba imetoa nafasi kwa kushirikisha Sekta ya Umma, Binafsi pamoja na Jumuiya za Kimataifa katika utekelezaji wake, bali pia imetoa nafasi kwa washirika wote hapa Zanzibar.

Vile vile, Sera hii ya Nishati imezingatia matakwa ya sera zetu zote hapa nchini kwa madhumuni ya kuleta ufanisi wa pamoja. Mhe. Spika, takriban sekta zote za Zanzibar zimepewa majukumu fulani, ili kuhakikisha sera hii imefanikiwa kiutekelezaji, kwa vile imepata nafasi ya kupata mapitio ya kila baada ya miaka mitano kutegemea na matakwa ya hali halisi. Hayo yameelezwa kwenye ukurasa wa 49. Kwa hivyo, itakuwa ni dira inayokwenda na wakati.

Mhe. Spika, napenda kuelezea kuwa Sera hii ya Nishati ni matarajio ya Wazanzibari. Kwa hivyo, kwa heshima kubwa kabisa ni imani yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu watatoa michango yao, ili kuifanya sera hii iwe imara zaidi na kupata ridhaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mwisho naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wote pamoja na watendaji wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, washirika wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika utaratibu wa kutayarisha sera hii. Vile vile, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza hili tukufu pamoja na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa miongozo yao adhimu katika kufanikisha uwasilishwaji wa sera hii mbele ya Baraza lako hili *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nawashukuru sana *(Makofi)*.

Mhe. Hamad Masoud Hamad (Waziri Kivuli Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi) Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Sera ya Nishati ya Zanzibar kama ifuatavyo:-

Mhe. nianza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW), Muweza wa yote na Bwana wa Ulimwengu huu, kwa kutuwezesha kukutana tena leo kujadili Sera ya Nishati, tukiwa wazima, wenye afya njema na wenye furaha.

Tumuombe Mwenyezi Mungu atupe hekima, busara, upeo na atuongoze vyema katika kujadili jambo hili muhimu sana kwa nchi yetu, kama vile alivyotuongoza wakati wa kujadili suala la mapendekezo ya serikali juu ya Uendeshaji wa kazi za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Zanzibar, hatimaye kufikia maamuzi yaliyompendeza kila Mzanzibari halisi, kiasi ambacho kila Mjumbe wa Baraza lako hili Tukufu anajipongeza kwa mafanikio makubwa yaliyofikiwa. Sasa Mafuta na Gesi Asilia, Zanzibar ni ya Wazanzibari wenyewe. Hivi ndivyo tulivyotaka na ndivyo imeshakuwa *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kwa miaka minne mfululizo tangu mwaka 2006, kama msemaji rasmi wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Maji Ujenzi Nishati na Ardhi katika Hotuba zote za Bajeti nimekuwa na wimbo wa madai ya kuhimiza kuwa na Sera ya Nishati ya Zanzibar. Hatimaye leo Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wanajadili sera hiyo.

Mhe. Spika, niruhusu nimpongeze Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Mhe. Naibu Waziri, pamoja na watendaji wake katika Wizara na Idara ya Nishati kwa kutimiza ahadi yao kwa Baraza lako Tukufu *(Makofi)*.

Mchakato wa kutayarisha sera hii umechukua muda mrefu na umegharimu fedha. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuru wafadhili waliosaidia kufanikisha sera hii.

Mhe. Spika, sera hii ni miongoni mwa sera chache zilizotayarishwa na kuandikwa kitaalamu, zilizowahusisha na kuwashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo Taasisi na Jumuiya kadha, Wizara za Serikali, na wataalamu muwafaka. Aidha njia zilizotumika za vikao, semina, warsha, midahalo, dodoso, kupata na kuangalia Sera za Nishati kutoka sehemu mbali mbali nazo zilichangia sana kuifanya sera hii kuwa ya kitaalamu zaidi.

Kwa kweli taarifa ya hivi sasa ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi imechangamsha ukumbi. Kwa hivyo, ukumbi huu naamini taarifa hii itasaidia pamoja na kurahisisha majadiliano ya sera hii *(Makofi)*.

Mhe. Spika, niruhusu tena kwa niaba ya Kambi ya Upinzani niwapongeze na kutoa shukurani maalum na za pekee kwa Serikali ya Norway, kwa kupitia kwa Shirika lake la Maendeleo *NORAD* na Balozi wake hapa Tanzania. Kwa kweli

jinsi walivyopania katika kuisaidia Zanzibar katika masuala ya Nishati ya Umeme na Mafuta na Gesi Asilia.

Vile vile, napenda kuwakumbusha Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwamba umeme vijijini ni wao, umeme wa Tanga hadi Pemba ni wao, vipuri kwa ajili ya mashine za umeme Pemba ni wao, na Semina Maalum juu ya Mafuta na Gesi iliyofanywa hivi karibuni katika ukumbi huu kwa ajili ya kuwapa taaluma Wajumbe wako pia ni wao *(Makofi)*.

Pamoja na hayo, hivi sasa taarifa ya Mhe. Waziri kuhusu kiasi gani Serikali ya Norway itasaidia utafiti wa mazingira katika masuala ya mafuta na gesi asilia inazidi kupamba. Kutokana na hali hiyo Serikali ya Norway imethibitisha kuwa imepania kweli katika kuisaidia Zanzibar kwenye masuala ya nishati *(Makofi)*.

Mhe. Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuiomba tena Serikali ya Norway, kutukamilishia usambazaji umeme katika vijiji vichache vilivyobaki kupata umeme. Vijiji hivi vinajiona kama watoto wa kambo waliokosa bahati na wanajiona kama vile wao hawapendwi kama wengine.

Mhe. Spika, Sera ya Nishati ya Zanzibar imetaja hoja 24, matamko 37 na jumla ya mikakati 83 na kueleza uhusiano wake wa karibu na sera za sekta nyengine za uwekezaji, Biashara, Mazingira, Kilimo, Maji, Ardhi, Misitu zote za Serikali ya Zanzibar. Lugha mbili, ile ya Kiswahili na ya Kiingereza zinatoa nafasi nzuri ya ufafanuzi wa yale yaliyoainishwa katika sera hii *(Makofi)*.

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo muhimu yasiyohitaji kusubiri na ya kuchukuliwa hatua muafaka hivi sasa ni haya yafuatayo:-

1. Kupambana na uwezo mdogo wa Idara ya Nishati kusimamia upatikanaji na ugavi wa nishati kulingana na mahitaji.

2. Kujenga uwezo wa Idara ya Nishati. Mhe. Spika, nafasi za masomo (mafunzo) ya Shahada ya kwanza (BSC), naya pili (MSC) katika nyanja mbali mbali, ambazo Wizara ya Maji, Ujenzi Nishati na Ardhi tayari wanazo ambazo ufadhili upo tayari, zifanyiwe kazi na vijana Wazanzibari na Wazalendo na wenye sifa zinazotakiwa wapatikane haraka kwenda kusomea fani hizo.

   Fani zenyewe ni *Petroleum Chemistry, Petroleum Engineering, Petroleum Geophysics, Geology, Petroleum Law, Energy Development Engineering, Petroleum Management, Human Resources Management na Petroleum Inspector*. Hizi ni jumla ya nafasi 39 za mafunzo *(Makofi)*.

Mhe. Spika, hivi sasa Idara ya Nishati kwa nishati ya mafuta ya *petrol*, *diesel* na *kerosene* inabaki kuwa mtazamaji tu, wala haikupewa dhamana kamili ya kudhibiti nishati hii. Kwa hivyo, tunashauri dhamana ya kujua wingi wa mafuta, upimaji wa ubora wa mafuta pamoja na masuala yanayohusiana na mafuta wapewe wao. Isipokuwa Wizara ya Fedha na Uchumi, wao waendelee kuwa na takwimu zao za wingi wa mafuta na malipo ya kodi yanayohusiana na nishati hii.

Mhe. Spika, Idara ya Nishati kwa kushirikia na Wizara ya Fedha na Uchumi katika masuala yote ya nishati ni jambo la lazima, vyenginevyo tatizo la Idara ya nishati ni kuwa hawapati na wala hawana taarifa nyingi muhimu litaendelea. Idara hii iwezeshwe kwa kupatia vifaa vya kisasa vya kupata wingi na ubora wa mafuta na hapo baadaye kuwa na maabara yake ya kupimia mafuta pamoja na mambo mengine.

3. Kushajiisha wananchi wengi kuunga umeme kwa matumizi ya nyumbani. Shirika la Umeme halina budi kupunguza masharti magumu na gharama za uungaji umeme majumbani, ambazo kwa sasa ni kubwa mno na zinakwaza juhudi za wananchi wanyonge kujiungia umeme ambao wanauhitaji kwa maendeleo yao *(Makofi)*.

4. Kwa kuwa nishati ya gesi kwa matumizi ya nyumbani ya kupikia inapatikana kwa wingi hapa Tanzania. Serikali ibuni vivutio kwa wale wanaotaka kufanya biashara ya kusambaza na kuuza gesi hiyo kwa wananchi. Kusambazwa kwa gesi hii, majumbani kwa gharama nafuu itapunguza sana matumizi ya kuni na mkaa. Kwa hivyo, itapunguza sana uharibifu wa misitu pamoja na mazingira.

5. Matokeo ya Mei 2008 na haya tunayoendelea nayo yaliyotokea tarehe 10/12/2009 ya kukosa umeme kwa karibu ya siku 40, leo yawe ni mafunzo tosha kwa Serikali. Hasara kwa uchumi wa serikali na ugumu wa maisha ya wananchi yako wazi.

   Serikali ipange mipango yake upya, ikate pua iunge wajihi kuhakikisha kwamba kunapatikana japo mashine mpya za umeme (*Generators*) zitakazokidhi japo nusu ya mahitaji ya matumizi kwa hapa Unguja na huko Pemba. Pamoja na kwamba kuna miradi mipya ya kupatikana kwa umeme kutoka Tanzania Bara kwa kutumia waya wa baharini (*submarine cable*) inayofadhiliwa na *NORAD* kwa Pemba na MCC kwa Unguja.

6. Kutokana na kukosekana kwa Nishati ya Mafuta ya mara kwa mara hapa Zanzibar na pamoja kwamba kuna wawekezaji kadha waliopewa jukumu la kuipatia mafuta Zanzibar. Hivi sasa wakati umedhihiri wa serikali kuwa na akiba yake wenyewe (*reserves*) ya mafuta hayo endapo hali hiyo itakuwa inajitokeza iweze kudhibitiwa *(Makofi)*.

7. Serikali iwahamasishe wawekezaji kujenga *Oil Depot*, kwa ajili ya kuhifadhi shehena kubwa ya aina zote za mafuta kwa ajili ya biashara za kimataifa na kwa matumizi ya hapa nyumbani.

Mhe. Spika, niruhusu nimpongeze mwekezaji mwenyeji na Mzanzibari halisi anayemiliki Kampuni ya *Ocean Petroleum* anayejenga *Depot* kubwa ya mafuta huko Mangapwani, Wilaya ya Kaskazini B, Unguja *(Makofi)*.

Mhe. Spika, mimi Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wa Baraza hili, nimeshiriki kwa kiwango kikubwa katika matayarisho ya Sera hii ya Nishati pamoja na Wajumbe wengine wa Kamati. Hivyo, nawaomba Wajumbe wenzangu wa Baraza hili nao waijadili kwa makini hasa katika hoja zifuatazo:-

- Kupunguza matumizi ya nishati inayotokana na kuni na mkaa.

- Uhakika, urahisi na kujitegemea kwa upatikanaji wa nishati ya umeme na mafuta.

- Uimara wa Shirika la Umeme na Idara ya Nishati.

- Kupunguza utegemezi wa nishati kutoka nje.

- Nishati mbadala.

Mhe. Spika, kwa furaha kubwa na imani ndani ya roho yangu naunga mkono Sera ya Nishati Zanzibar. Vile vile, naheshimu sana michango itakayotolewa na Wajumbe wa Baraza lako wakati wa majadiliano, pia ninaamini Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake watafarijika sana na michango hiyo adhimu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Sera ya Nishati Zanzibar iko mezani kwa ajili ya kujadiliwa ni jambo muhimu ambalo ni kubwa ningetemegea ukumbi huu ujae ili tuichangie kweli, kwa ajili ya kusaidia wizara katika

kufanikisha suala hili. Kutokana na hali hiyo, kama vile tulivyochangia masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, basi hili ni sambamba na lile *(Makofi)*.

Kwa hivyo, niko tayari kutoa muda tumalize shughuli zetu mapema leo, kwa ajili ya kuweza kupata kuipitia vizuri baada ya kuwasilishwa ili Jumatatu tuje na nondo kamili kwa lengo la kuchangia vizuri kabisa pamoja na mimi. *(Kicheko/Makofi)*.

Waheshimiwa Wajumbe kwa rai hiyo ambayo nimeitoa basi nimuombe Mhe. Waziri awaombe Wajumbe kufanya hivyo. Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha.

KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha: Mhe. Spika, kwa vile umetupa kazi ya kwenda kujitayarisha vizuri kwa ajili ya kuja kuichangia vizuri Sera hii ya Nishati siku ya Jumatatu, basi naomba kutoa hoja kwamba uliahirishe Baraza hili kabla ya wakati wake hadi siku ya Jumatatu, tarehe 24, Januari 2010 saa 3:00 asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubalia na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda *(Makofi)*.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijaahirisha kikao hiki, pale kipindi cha asubuhi muda ulimalizika kabisa. Lakini niliombwa nitangaze kwamba leo hii kunafunguliwa, yaani ni ufunguzi rasmi wa Kombe la Marehemu Sheikh Thabit Kombo, mchezo wa ufunguzi huo utafanyika hapo katika uwanja wa Mao-Tse-Tung, mechi zitakuwa zikiendelea hadi tarehe 8, mwezi wa Febuari mwaka huu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo aliniomba nitoe taarifa hiyo na shughuli hii ilikuwa ifanyike hivi saa 10 jioni muda ambao

umeshapita kidogo. Kwa hiyo, naomba nichukue fursa hii kutoa taarifa hiyo kwenu, lakini mechi hizo zitakazoendelea zisije kuharibu shughuli zetu za kikao na mkutano huu unaoendelea.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa naahirisha kikao hiki hadi tarehe 25 mwezi wa Januari mwaka 2010 siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 11:55 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 25/01/2010 saa 3:00 asubuhi)